# Nipashe

Jumamosi Mei 18, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581680

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11

**Ziara** ya Rais Samia Ufaransa yazaa matunda

UKURASA 3

**Makonda** asema anaogopa kurudi mtaani, ni kugumu

UKURASA 4

**Wadau** wasema Watanzania bado wanahitaji Katiba Mpya kwa amani

UKURASA 5

# Askofu Mkuu ajinyonga kisa madeni na mgogoro

UKURASA 2





Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu akiwaonyesha waandishi wa habari na wanachama wa chama hicho, matundu ya risasi kwenye gari lake, baada ya kukabidhiwa katika Kituo Kikuu cha Polisi cha Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Tundu Lissu akabidhiwa gari baada ya miaka saba

UK. 4

# Wabunge wacharuka ushoga, ulawiti, ndoa za jinsia moja



- **Wataka** sheria makosa kujamiiana ifumuliwe, wahusika...

*Endelea ukurasa 2*

**MICHEZO** **SIMBA YAGOMEA DAU LA CHAMA** UK.24

**MAONI,** UK.6

## Kikwete ataka viongozi kuacha alama kazi zao

**Na Beatrice Shayo**

RAIS Mstaafu, Jakaya Kikwete, amewashauri waliohitimu uongozi kuwa na mipango na mawazo yatakayowawezesha kuacha alama katika uongozi wao pale watakapomaliza muda au kuhamishwa.

Kikwete aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika mahafali ya saba wakati akiwatunuku astashahada na vyeti wahitimu 198 katika Taasisi ya Uongozi.

Alisema ni lazima viongozi wawe na mipango kabambe kwa taasisi zake ili mwisho wa siku wakumbukwe kwa alama watakazoziacha.

"Watu watakukumbuka kwa lipi katika uongozi wako. Tujitahidi kuacha alama," alisema.

Kikwete alisema katika kutekeleza majukumu yao, viongozi wanapaswa kuwa vyanzo vya mawazo na mawakala wa mabadiliko katika ngazi za awali.

"Lazima wawe tayari kila wakati kutafuta suluhu za changamoto zinazoendelea kama vile umaskini, mabadiliko ya tabia nchi, ujinga, shida ya chakula, magonjwa na mambo mengine wajikite kutatua kero zinazojitokeza,"alisema Kikwete.

Aidha, Kikwete alionya kuhusiana na tabia zinazoibuka za kuwatelekeza watoto wa kiume na kuwaendeleza wasichana akieleza kuwa wazazi wana jukumu la kutengeneza uwiano.

Alisema wavulana na wasichana lazima walelewe kwa usawa katika elimu na wale wanaohusiana na hilo ili kuziba pengo.

Kikwete aliipongeza Taasisi ya Uongozi kwa mchango wake endelevu wa kuwaandaa na kuwapa ujuzi viongozi.

Naye Waziri wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, alisisitiza uadilifu na uwajibikaji kwa viongozi huku akiwakumbusha kuwa mabalozi wazuri wa taasisi hiyo na kujituma katika kuwatumikia wananchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Uongozi, Kadari Singo, alisema programu hizo zilitoa jumla ya wahitimu 198 ambao walikamilisha programu zao za muda mrefu za utendaji katika Stashahada ya Uzamili ya Uongozi (PGD), Vyeti vya Uongozi (CiL) na Mpango wa Uongozi wa Wanawake (WLP).

Alisema programu hizo zinalenga kukuza uwezo wa uongozi katika uongozi binafsi, watu na shirika.

Singo alisema kuwa programu hizo ni maalum kwa ajili ya viongozi wanaotaka kukuza maendeleo yao kitaaluma bila kuweka taaluma zao.

Katibu Mkuu Kiongozi wa Zanzibar, Mhandisi Zena Ahmed Said, aliipongeza Taasisi ya Uongozi kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Aalto cha Elimu na Maendeleo ya Taaluma (Aalto EE) cha Finland.

Alisema kuwa mafunzo ya uongozi yatajenga na kuboresha utendaji wao kwa kuwa mafunzo hayo yanaongeza ujuzi kwa viongozi ya namna wanavyoweza kufanya vyema sehemu zao za kazi.

Mhandisi Said aliipongeza Taasisi ya Uongozi kwa kutambulisha wanawake katika programu za uongozi na kuongeza kuwa inaboresha uwezo wa washiriki wa kusimamia nafsi zao za ndani, kuongoza wengine na kutumia rasilimali vizuri.

# Askofu ajinyonga kisa madeni, mgogoro

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Methodist Tanzania, Joseph Bundala (55), amekutwa amejinyonga kwa kamba ndani ya ofisi yake iliyoko kwenye kanisani hilo, Mtaa wa Meriwa, jijini hapa.

Kiongozi huyo wa kiroho, ameacha waraka mrefu ukieleza sababu za kuchukua uamuzi huo kuwa ni madeni na mgogoro ulioko katika uendeshaji wa shule binafsi.

Bundala ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Kanisa hilo kwa Afrika, mwili wake uligundulika juzi saa 1:00 usiku ukiwa unaning'inia ofisini kwake.

Akizungumzia tukio hilo jana, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Alchelaus Mutalemwa, alisema Jeshi la Polisi linachunguza tukio la askofu huyo, ambaye ni Mkazi wa Ihumwa jijini hapa kuchukua uamuzi huo.

"Tukio hilo liligundulika Mei 16, 2024 majira ya saa 1:00 usiku katika mtaa wa Meriwa, Dodoma, ndani ya ofisi yake iliyoko katika kanisa hilo. Uchunguzi katika eneo la tukio umekutwa ujumbe unaeleza sababu za kujinyonga ni madeni na mgogoro uliopo katika uendeshaji wa shule binafsi," alisema.

Alisema taarifa za awali hazijaeleza kiasi anachodai au kudaiwa kupitia ujumbe aliouacha.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa Mtaa wa Sulungai, Grevas Lugunyale, alisema alipigiwa simu na mchungaji wa kanisa hilo kwa madai kuwa wamekuta Askofu amejinyonga.

"Nilipiga simu polisi kutokana na kukutwa amejinyonga. Katika ukaguzi tulikuta mezani kuna waraka ameuandika yeye mwenyewe. Kuna madai anadai na kuna madai naye anadaiwa. Polisi walipokuja pia walifanya uchunguzi wao tukahojiwa na kuchukua mwili kwenda kuuhifadhi," alisema.

Alisema tukio kubwa na linaumiza kwa kuwa ni Askofu ambaye watu wengi wanamuamini na wanamjua lakini inaonekana hakuwa na watu wa kuwaambia yaliyomsibu ili apate ushauri ambao ungemsaidia.

Mwenyekiti wa Shina Namba 11, Jonathan Mpando, alisema anamfahamu Askofu Bundala amekuwa akisaidia kwenye kampeni kutokana na kuwa na kundi kubwa la waumini.

Jirani wa Askofu huyo, Kedmond Ngalya, alisema amejinyonga akiwa ofisi kwake na kuacha waraka ambao ulichukuliwa na polisi.

Naye jirani mwingine, Omar Hussein, alisema siku tatu zilizopita alikutana na Askofu huyo na walisalimiana na hakuonyesha dalili zozote za kukatisha maisha yake.

"Ila nimeshangaa taarifa ya kujinyonga kwake usiku ya jana (juzi) kusikia Askofu anayekemea dhambi ya kujinyonga na yeye amejitundika kwa kamba," alisema.

Steve Magawa ambaye ni Jirani, alisema kifo hicho kimemsikitisha kwa kuwa kiongozi huyo wa dini alikuwa mwalimu wa matendo ya Mungu.

Katibu Mkuu wa Kanisa hilo, Allen Siso, alisema alipigiwa simu majira ya saa nne na mmoja ya watumishi na kwamba taarifa zaidi wataeleza baada ya kukaa kikao.



Wafanyakazi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), wakizibua mtaro wa maji machafu katika Barabara ya Morogoro, eneo la Lumumba, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wabunge wacharuka ndoa jinsia moja

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WABUNGE wamecharuka bungeni kuhusu vitendo vya mapenzi ya jinsia moja, ushoga na kukithiri kwa ubakaji na ulawiti nchini huku wakipendekeza watakaobainika wahasiwe.

Aidha, wamependekeza serikali ipeleke bungeni marekebisho ya Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ya Mwaka 1998 ili kuongeza adhabu kwa washtakiwa na kuondoa dhamana.

Akichangia jana bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mbunge wa Tarime Vijijini (CCM), Mwita Waitara, alihoji serikali inapata kigugumizi gani kueleza mikakati inayofanya ya kukabiliana na ushoga na kwamba watanzania hawapendi tabia chafu.

"Haiwezekani mtu anapinga mila zetu, anataka tufanye ushoga. (Dk. Harrison) Mwakyembe (aliyewahi kuwa Waziri wa Katiba na Sheria) na mwenzake wametangaza hadharani wametuonyesha ndoa za jinsia moja kati ya mwanamume na mwanamume, wanawake kwa wanawake lakini Waziri amekuja hapa hasema kama ni shida ya taifa.

"Hayati Mwalimu Julius Nyerere kama angekubali ushoga nchi isingefika hapa, hivyo kama kuna mpango wa kuua Watanzania ni vyema waziri mwenye dhamana akajiangalia kwa kuwa ushoga unachukiwa sana," alisema.

Alishauri nchi kurudi kwenye hoja ya kitaifa ya kupinga ushoga na ulawiti kama ni mwanaume aoe mwanamke kwa utaratibu na kama ni mwanamke aolewe na mwanaume.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Dk. Thea Ntara, alisema suala la maadili kumomonyoka limejipenyeza kwenye maeneo ya ushoga, ulawiti na ubakaji na kwamba adhabu zinazotolewa bado ni ndogo.

Alitaja matukio mbalimbali ya ulawiti kwa mwaka huu katika eneo la Bunju mtoto wa miaka nane wa kiume amelawitiwa, mwezi Machi mtoto wa kike alilawitiwa na mwalimu huku mke alipewa adhabu ya kulawitiwa kila akifanya kosa kama dhabu.

"Nawapa takwimu ili tupate uchungu, tusimame tukatae haya mambo, tuone hayafai. Ufukwen i sasa hivi watu wanalawitiwa huko kweye maji ndiko michezo inayofanyika. Watoto wenye walemavu ambao hawawezi kwenda popote inakuwa rahisi kubakwa na kulawitiwa,"alisema.

Pia alisema shuleni kumeharibika kwa kuwa michezo ya kulawitiana, kusagana hasa shule za mikoa ya Morogoro, Dar es salaam na Dodoma imeshika kasi.

"Ndiyo maana tunasema adhabu ya kumfunga mtu miaka 30 na kumwacha ndani bado anapata zile hisia na kule gerezani si ajabu atawabaka wale wafungwa adhabu ile imepitwa na wakati, leteni muswada bungeni hapa hatutaki mambo ya miaka 30 waje hao tuwahasi ili na wao wakae tu,"alisema.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mwantumu Dau Haji, alishauri itungwe sheria ili wanaobainika kuwa wamehusika kwenye ubakaji na ulawiti wahasiwe kwa kuchomwa sindano.

"Hotuba iliyosomwa na wizara ni nzuri sana lakini bado haijawa na mustakabalii wa kukomesha vitendo wanavyofanyiwa watoto nchini ikiwemo kubakwa na kulawitiwa, sheria iletwe hapa bungeni tuipitishe wote bungeni ili hawa watu wabakaji wahasiwe, watu hawa wametubakia watoto wetu," alisema.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Ng'wasi Kamani, alitaka kupitiwa kwa adhabu zinazotolewa kwa washtakiwa hao kwa kuwa adhabu ya miaka 30 inaonekana haifanyi kazi na kufutwa kwa dhamana kwa watuhumiwa wanaoshtakiwa kwa makosa hayo huku akipendekeza wazazi watakaofuta kesi za watoto wao wapewe adhabu kwa mujibu wa sheria.

Naye Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Kabula Shitobelo, alisema watoto wa kiume malezi yamekuwa ni tabu sana kwakuwa wakifika darasa la saba wazazi wanawaza wawapeke shule za bweni.

"Kuna baadhi ya mitandao inachochea masuala haya ya ushoga kama tusipokemea na kuweka sheria na adhabu kali tatizo litaendelea kusumbua nchi,"alisema.

## HABARI KITAIFA

# Ziara Rais Samia Ufaransa yazaa matunda

**Na Romana Mallya**

ZIARA ya Rais Samia Suluhu Hassan, aliyoifanya hivi karibuni Paris, Ufaransa, imezaa matunda baada ya serikali kueleza itakavyotekeleza mikakati yake kuhakikisha kila Mtanzania anakuwa na uwezo wa kupata nishati safi ya kupikia kwa gharama nafuu.

Rais Samia Mei 14, mwaka huu, alishiriki Mkutano wa Kimataifa ambao ulikuwa unahusu Nishati Safi ya Kupikia, akiwa kinara kwa upande wa Afrika na mwenyekiti mwenza wa mkutano huo.

Miongoni mwa mafanikio makubwa ya mkutano huo ni ahadi za serikali mbalimbali, washirika wa maendeleo na sekta binafsi zimeahidi kukusanya Dola za Kimarekani bilioni 2.2 huku Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ikiahidi kutoa Dola bilioni mbili kwa ajili ya nishati safi ya kupikia kwa kipindi cha miaka 10.

Akizungumzia ziara hiyo jana Ikulu jijini Dar es Salaam na mikakati ya nchi mawaziri wenye dhamana hiyo ni pamoja na kuendelea kuboresha miundombinu na kutoa elimu zaidi kwa wananchi kufahamu umuhimu wa nishati safi na kuachana na nishati isiyo salama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, alisema Rais Samia ameliheshimisha taifa na kuwataka Watanzania kutembea kifua mbele kwa kuwa, ajenda hiyo ya nishati safi si ya Afrika peke yake bali pia nchi mbalimbali.

"Ajenda ya Nishati Safi ilianza mwaka 2022 na mwaka jana iliendelea kwa upana zaidi. Kwa hiyo kwa Tanzania kuna mkakati uliokwishazinduliwa, ukionyesha utayari wa nchi katika hili," alisema.

Alisema uharibifu wa kimazingira kwa sasa kwa mwaka ni hekta 412, 000, hivyo moja ya mikakati ni kupunguza uharibifu wa kimazingira kwa kuhamia kwenye nishati safi ya kupikia, ili uharibifu huo usiendelee.

Pia alisema mkakati mwingine ni kuifanya serikali kila mwaka kupitia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM, kila halmashauri ipande milini 1.5, ili kupanda miti milioni 276 ambapo kwa mwaka 2023/24 imepandwa karibu 266.

"Lengo ni tuhamie katika ajenda yetu ya nishati safi ya kupikia kwa lengo la kulinda nchi. Kuhusu utafiti zipo nyingi tunashukuru sekta binafsi, alisema.

Jafo alisema lengo ni kuhakikisha mtanzania anaweza kununua kuhimili gharama za gesi kwa bei nafuu zaidi ya sasa.

Alishukuru vyombo vya habari kwa kazi kubwa inayofanya ya kuhakikisha watanzania wanaendelea kuelimika kuhusiana na matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Kuhusu gharama za matumizi ya nishati safi ya kupikia, Naibu Waziri Wizara ya Nishati, Judith Kapinga, alisema kuwapo kwa ruzuku kunalenga kuzipunguza kwa kuwa gharama ni changamoto.

"Kama serikali tumeanza kufanya kazi na tunaendelea nayo ndiyo maana msingi wa mkutano huu wa Paris. Kabla ya mkutano huu, Rais alizindua mkakati wa nishati safi ya kupikia ambapo mkakati wake ni ifikapo 2033/34, zaidi ya asilimia 80 ya watanzania wawe wanaitumia," alisema.

Hata hivyo, alisema hawatafikia huko kama hawatalizungumzia suala hilo pamoja na gharama ili kupungua.

"Ukitaka kupunguza gharama lazima tuboreshe miundombinu ya gesi safi ya kupikia na ni suala ambalo tayari tunalitazama.

"Kupitia Shirika la Petroli Tanzania (TPDC) tunayomikakati ya kuboresha ya upokeaji wa gesi bandarini, tunaamini ukipokea kwa kiasi kikubwa bandarini, itakuwa na uhusiano wa moja kwa moja na gharama kwa mlaji. Tumeanza kulifanyia kazi na kuliwekea misingi kwa kushirikiana na wadau," alisema.

Jambo lingine alilitaja ni gharama ya matumizi kwa mlaji wa kwanza akifafanua kuwa, changamoto kubwa ni mwananchi kuanza matumizi ya gesi ambapo mwanzoni lazima awe na vitendea kazi.

Alisema suala la kuangalia namna ya kuwaleta watanzania kwenye matumizi ya kwanza wameliangalia na kuweka mikakati na kuanza kulifanyia kazi.

Kapinga alisema kupitia Rais Samia kuna jambo ambalo ameiambia dunia kuwa mwaka 2024 ni wa kuleta mabadiliko mapya ya kupigania nishati safi ya kupikia kutokana na jitihada alizofanya.

Alisema katika mkutano huo masuala makubwa yaliyozungumziwa na Rais, aliiambia dunia ni lazima kuwapo programu mahsusi kwa Afrika na kuwa na rasilimali fedha.

"Tunamshukuru Rais kwa misingi hii aliyoweka ili dunia iwe na jicho la tofauti kwenye ajenda safi ya kupikia kwa Afrika. Maazimio yale na yaliyojadiliwa kwa sisi kama taifa tunampongeza," alisema.

Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Zuhura Yunus, alitaja mafanikio mengine ya mkutano huo ni nchi mashirika na kampuni 130 zimeidhinisha Tamko la Viongozi wa Juu wa kuipa Kipaumbele Nishati Safi ya Kupikia.

Alisema tamko hilo linadhihirisha nia ya kuchukua hatua kwa pamoja na ushirikiano wa kushughulikia ukosefu wa upatikanaji wa nishati safi ya kupikia.

"Mkutano huu uliandaliwa na Shirika la Nishati Duniani, IEA ambalo makao makuu yake yapo Ufaransa.

"Kutokana na mkutano huo, Rais wa AfDB, Dk. Akinwumi Adesina, amesema kuwa Rais Samia amedhihirisha kuwa yeye ni kiongozi mahiri (a great leader) kwa kufanikisha mkutano huo akiwa kama Mwenyekiti Mwenza, ambapo zaidi ya Dola za Marekani bilioni 2.1 ziliweza kupatikana papo kwa papo kutokana na nguvu kubwa ya ushawishi ya Rais Samia," alisema.

Katika mkutano huo, Dk. Adesina alisema kuwa, Rais Samia ni kiongozi wa kuenzi kwenye Bara la Afrika kama vito, kwa maneno yake akimwelezea kama "a gem for Africa".

Pembezoni mwa mkutano huo Rais Samia alifanya mazungumzo ya uwili na Rais Emmanuel Macron yakilenga umuhimu wa kuimarisha ushirikiano katika maeneo ya nishati (safi), maji na uwezeshaji wa wanawake.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions ndio uende "pay via mobile". Itakuletea maelekezo namna ya kulipa kwa simu kulingana na mtandao unaotumia.
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia
6. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

7. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-6



Kwa mawasiliano zaidi Tupigie: 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Barua pepe: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian



Wafanyabiashara wadogo maarufu machinga wakifanya shughuli zao chini ya transfoma ya kupooza umeme mkubwa katika makutano ya mitaa ya Tandamti na Nyamwezi, eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana, kitendo kinachoweza kuhatarisha usalama wa maisha yao na wateja endapo itatokea hitilafu. **PICHA: JOHN BADI**

# Makonda asema anaogopa kurudi mtaani, ni kugumu

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda amesema anatambua "mtaani ni kugumu" na asingependa arejee tena katika maisha bila ajira.

Makonda ana uzoefu wa kukaa nje ya mfumo wa ajira serikalini na chama (CCM), akikaa nje ya mfumo huo kuanzia Julai 15, 2020 Rais John Magufuli alipomwondoa kwenye nafasi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam hadi Oktoba 22, 2023 CCM ilipomteua kuwa Katibu wa Halmashauri Kuu ya chama - Itikadi, Uenezi na Mafunzo.

Amesema anahitaji msaada wa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi kutekeleza majukumu aliyoagizwa na Rais Samia Suluhu Hassan mkoani Arusha.

Makonda alitoa kauli hiyo jana wakati wa semina ya uwekezaji na elimu ya fedha iliyoandaliwa na Benki ya CRDB kwa wanahisa wake na Watanzania kuelekea Mkutano Mkuu wa 29 wa Wanahisa wa benki hiyo unaofanyika leo katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC), jijini Arusha.

Alisema kuwa ameagizwa na Rais Samia kuhakikisha anachochea kasi ya uwekezaji katika sekta ya utalii ili kuongeza wageni wanaotembelea mkoa huo.

Makonda, aliyewahi kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni (kuanzia Februari 19, 2015 akiteuliwa na Rais Jakaya Kikwete hadi Machi 13, 2016 alipoteuliwa na Rais Magufuli kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, alisema asipenda kuona familia yake ya watoto watatu inapata tabu.

"Mimi ninavyokufahamu wewe Mheshimiwa Rais Mwinyi, ni rafiki yangu, wewe ni rafiki wa watu wengi wema, Makonda alisema. Mimi nina maombi mawili tu. Arusha na Zanzibar hatuwezi kukwepana, watalii wanaotua Zanzibar ndiyo hao wanaokuja kutua Arusha.

Ombi langi la kwanza, nifikishie salamu zangu za upendo wa watu wa Zanzibar, waambie kila wanapopata mtaalii - iwe ni Unguja, iwe ni Pemba, waambie wasiishie pale, waje wamtembee ndugu yao ambaye yuko Arusha.

La pili, Mheshimiwa Rais, unafanya kazi kubwa sana kule Zanzibar, kila siku unafungua hoteli, na mimi nimepewa hii ajenda na Mheshimiwa Samia, watoto wangu - ninao watatu, mkubwa ana miaka mitano, wale pacha wana umri wa miaka mitatu, nilishakaa mtaani nikaona hali ya mtaani.

Rais amenipa agizo kuchochea utalii, kasema 'kahakikishe unaongeza vyumba'. Usiponishika mkono wewe kaka yangu Mheshimiwa Mwinyi, nitapata wapi wawekezaji wa kujenga hoteli katika mkoa wangu wa Arusha?

Kwa unyenyekevu mkubwa ninakuomba, wale wanaojenga hoteli Zanzibar, waambie una mdogo wako Makonda, yuko Arusha, ili wale wawekezaji kutoka huko duniani wakatua Zanzibar, basi wakija, wawe na matawi yao mkoani Arusha kuendeleza shughuli za utalii," alisema.

Katika hotuba yake ya kufungua semina hiyo, Rais Dk. Mwinyi alijibu maombi hayo ya Makonda, alisema ombi lake la kwanza tayari linafanyiwa kazi.

Alisema ni ukweli usiofichika kwamba watalii karibu wote wanaokuja Tanzania, ni ama wanaanzia Tanzania Zanzibar kish wanakwenda Arusha au wanaanzia Arusha kisha wakwenda Zanzibar.

"Kwa hiyo, hili linafanyika, Ninaweza kukuhakikishia leo ukitaka kupata ndege ya kwenda Zanzibar kutoka hapa Arusha inabidi ukate mapema sana kwa sababu wasafiri ni wengi. Ombi hili tayari linatekelezwa.

"Lakini lile la uwekezaji sasa, kwamba wawekezaji wanaojenga hoteli, na ni kweli kule Zanzibar sasa hivi tumepata neema ya uwekezaji mkubwa katika sekta ya utalii, hoteli nyingi zinajengwa, na zingine zinajengwa katika visiwa vidogo.

"Hivi karibuni tutafungua ya kwanza, Juni Mosi mwaka huu tutafungua hoteli ya kwanza iliyojengwa katika kisiwa. Ni ya aina yake kwa kweli! Sasa hawa tuko tayari kuwashawishi waje kuwekeza na upande wa pili ili mnyonyoro wetu huu wa utalii uendelee.

"Ni ama waanze kwenye safari wamalizie kwenye fukwe au waanze kwenye fukwe wamalizie kwenye safari huku. Hili ni jambo ambalo tupo pamoja Mhehimiwa Mkuu wa Mkoa (Makonda)," Rais Dk. Mwinyi aliahidi, akiomba wanahisa wa CRDB mkutano wao wa 30 mwakani ufanyike Zanzibar.

Katika salamu zake, Makonda pia alisema wanatekeleza kwa kasi mradi wa ujenzi wa kisasa wa soka mkoani Arusha ambao serikali imetoa zabuni ya Dola milioni 112 (Sh. bilioni 286).

Katika kutekeleza maagizo ya Rais Samia - kuchochea utalii mkoani Arusha, Makonda alisema wana mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoa vifaa vya kulisaidia Jeshi la Polisi kuimarisha usalama; ameahidi kulipa jeshi hilo magari 20, pikipiki 50, baiskeli za umeme 100.

"Baada ya miezi mitatu minne ijayo ukija Arusha utakutana na polisi wa utalii, vijana wazuri, wenye uwezo wa kuongea lugha zote mbili; Kiingereza na Kiswahili.

"Watamkaribisha mtaalii vizuri. Ninawashukuru CRDB kwa kutuunga mkono katika kuwezesha upatikanaji vifaa hivi. Asiyetambua kule alikoshikwa mkono, hawezi kutambua anakoelekea," alisema.

## Lissu akabidhiwa gari baada ya miaka saba

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amekabidhiwa rasmi gari lake ikiwa ni miaka saba tangu ashambuliwe kwa risasi na watu wasiojulikana huku akitamani kulipeleka Makumbusho ya Taifa.

Gari hilo, aina ya Toyota Landcruiser V8 VXR, lilikuwa limehifadhiwa kwenye Kituo Kikuu cha Polisi cha Dodoma tangu Septemba 7, 2017 lilipotokea tukio hilo nyumbani kwake, Area D jijini hapa.

Akizungumza jana baada ya kukabidhiwa gari hilo na Mrakibu Mwandamizi wa Polisi (SSP) Daniel Bendarugaho, mwanasiasa huyo alisema kama ingekuwa mapenzi yake, angetamani liwekwe makumbusho jinsi lilivyo bila kufanyiwa matengenezo lakini anahitaji usafiri kwa kuwa anatumia magari ya kuazima.

"Lakini nahitaji usafiri na magari ya kuazima azima pamoja na wema wa wanaowaazima sitaki kuwachosha sana, hivyo tutatengeneza ili ifanye kazi. Nitapendekeza liwekwe kwenye makumbusho ya nchi lakini kama wakubwa watasema hawataki kukaa na ushahidi wa namna hii tutatengeneza utaratibu wa kuhifadhi katika makumbusho binafsi," alisema.

Lissu aliwashukuru wanachama wa chama hicho kwa misaada na kuwa pamoja naye kwa kipindi chote tangu kutokea tukio hilo.

Alisema katika risasi zilizopigwa kwenye gari hilo ziliingia maeneo mbalimbali ya mwili na kwamba hadi sasa bado anatembea na risasi mgongoni.

"Mungu ni mwema bado nipo hapa, sasa hili gari tunachukua tukatengeneze tubadili milango, tutalihifadhi mahali gari lilikuwa jipya. Hili halijaharibika sana linahitaji kutengenezwa ili lifanye kazi. Tuna kazi kubwa ya kufanya kama mnavyofahamu.

"Litafanyiwa matengenezo lirudi kazini na siku ikifika haiwezi kufanya kazi basi tutarudishia hii milango tutafanya utaratibu iwekwe kwenye makumbusho ili watakaokuja baada yetu waje wajue kuna tukio baya liliwahi kutokea,"alisema.

Lissu aliwaomba watu wema waliomsaidia wakati wa matibabu, wamsaidie kutengeneza gari hilo ili lifanye kazi.

"Vilevile baadae nitaomba msaada utakapofika wakati wa kupelekwa kwenye makumbusho likawe somo kwa watoto wetu na wao watakaokuja baada ya sisi,"alisema.

Lissu alishukuru Jeshi la Polisi kwa kutunza gari hilo licha ya kuwa na eneo dogo la kuhifadhi vielelezo vya uhalifu.

## Msigwa, Sugu rasmi Nyasa

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimetoa baraka kwa Joseph Mbilinyi (Sugu) na Peter Msigwa, kupambana kwenye sanduku la kura katika uchaguzi wa mwenyekiti wa chama hicho Kanda ya Nyasa.

Awali, kulikuwa na tetesi kwamba huenda mmojawapo 'angekatwa' baada ya usaili uliofanywa na Kamati Kuu uliofanyika kwa siku nne kuanzia Mei 11, mwaka huu.

Jana, chama hicho kilitoa orodha ya majina ya walioteuliwa kwenda kupambana kwenye sanduku la kura katika kanda zao, huku Sugu na Mchungaji Msigwa ambao wote waliwahi kuwa wabunge, yakipenya.

Kanda hiyo ndiyo imeonekana kuwa na ushindani mkubwa kuliko kanda zingine na kumekuwa na kupigana 'vikumbo' vya hapa na pale miongoni mwa vigogo hao machachari wa CHADEMA pamoja na wafuasi wanaowaunga mkono kila upande ukitumia mbinu kujigamba.

Walioteuliwa kugombea katika kanda zingine ni Hezekiah Wenje ambaye aliwahi kuwa Mbunge wa Nyamagana na John Pambalu, Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la Chama hicho (BAVICHA).

Katika orodha hiyo ya wagombea iliyotolewa jana, wamo baadhi ya waliokatwa akiwamo Emmanuel Ntobi, aliyekuwa akiwamia uenyekiti Kanda ya Serengeti, ambaye kwa sasa ni mwenyekiti wa chama hicho mkoa wa Shinyanga na mwenzake James Mahangi.

Kwa Kanda hiyo ya Nyasa wagombea walikuwa watatu na mmoja akiwamo Daniel Mwambipile, ambaye amekatwa.

Kanda ya Magharibi, wagombea wote wanne wameteuliwa ambao ni Dickson Matata, Gaston Garubindi, Mussa Mafure Na Ngassa Mboje.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje, John Mrema, Kanuni ya 7.5 ya CHADEMA yenye vipengele 13 inaeleza sifa ambazo kila mgombea kulingana na nafasi yake anatakiwa kuwa nazo na ndiyo iliyotumika kuteua wagombea hao.

Akizungumza na Nipashe hivi karibuni, Mrema alisema watia nia watakaokatwa itabidi wakubali matokeo kwa kuwa, zipo kazi nyingine za chama chao wataendelea kufanya.

"Maana ya usaili ni kwamba, tuna vigezo vyetu kwa mujibu wa Katiba na Kanuni yetu, ni sifa gani viongozi wa ngazi gani wanapaswa kuwa nayo.

"Kwa hiyo ndiyo maana kama mtu akikutwa hana hizo sifa, basi moja kwa moja anaweza akaenguliwa, akashauriwa atumikie majukumu mengine kwa sababu bado ni chama kimoja, nafasi ni chache, wanachama wote hawawezi kuwa viongozi," alisema.

Kwa mujibu wa Mrema, uchaguzi kwenye kanda hizo unatarajiwa kufanyika Mei 29, mwaka huu.

Kuhusu mambo mengine yaliyojiri kwenye kikao cha kamati kuu, anayesubiriwa ni Mwenyekiti wa Chama hicho Taifa, Freeman Mbowe, kuweka wazi wakati wowote.

# Wadau wasema Watanzania wanayo nafasi kupata Katiba Mpya na bora

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANASIASA, viongozi wa dini na wanaharakati wamesema Watanzania bado wana nafasi ya kupata Katiba Mpya yenye misingi madhubuti ya kuchagiza uimarishaji wa demokrasia.

Vilevile, wamesema suala hilo linaweza kufanyika kwa kujifunza mbinu walizotumia nchi za Kenya na Afrika Kusini.

Wadau hao waliyasema hayo jana visiwani Zanzibar katika mkutano wa siku mbili uliokuwa ukijadili dhana ya demokrasia jumuishi na shirikishi, wakisisitiza umuhimu wa kupatikana kwa Katiba Mpya yenye maoni ya wananchi.

Mkutano huo mbali na viongozi hao ulihudhuriwa na asasi za kiraia zikiwamo za nchini Kenya na Afrika Kusini, pamoja na maofisa wa kibalozi wa nchi mbalimbali washirika wa maendeleo wanaowakilisha nchi zao nchini.

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe, Dk. Benson Bagonza, alisema Tanzania inahitaji Katiba Mpya bila ya kumwaga damu, ili kuendelea kuhifadhi historia iliyotukuka na ya kipekee katika ukanda wa Afrika ya kupata uhuru kwa amani.

"Tulistahamili wakati wa vita baridi kati ya kambi za kiitikadi za mashariki na magharibi, tuliingia mfumo wa vyama vingi bila ya kumwaga damu, na tumeulinda Muungano wetu wa Tangayika na Zanzibar bila ya kumwaga damu

Alisema kwa sasa wanahitaji kupata Katiba Mpya bila ya kulazimisha watu kukata tamaa na kuingia katika vurugu.

Mwanaharakati wa Haki za Binadamu, Dk. Helen Kijo-Bisimba, mbali na kutambua umuhimu wa Tanzania kupata katiba mpya, alisema anaamini kwamba, hatua za kufikia kileleni lazima ziwe shirikishi na zinazotokana na mipango ambayo ni zao la wananchi na siyo kuongozwa na watawala.

"Suala hili liwe la watu wenyewe na liwe ni mchakato, siyo la kuletewa. Hapa kwetu mara nyingi tunaona mambo ya katiba yanaletwa na watawala. Wenzetu Kenya na Afrika Kusini suala hili lilihusisha watu wenyewe," alisema Bisimba, ambaye ni muasisi wa Kituo cha Sheria na Haki za Bnadamu (LHRC).

Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, alisema: "Kama Kenya walipata nguvu ya kujenga msukumo kutokana na ukabila na Afrika Kusini wakajenga msukumo kutokana na ubaguzi wa rangi, hivyo ni vyema Tanzania kujenga msukumo kutokana na umoja katika kupata katiba mpya."

Mbowe alisema siku moja wafanye maandamano kwa watanzania wanaohitaji katiba bora kwa ajili ya taifa, bila ya kujali chama wala dini.

Alisema ni vyema kuunganisha nguvu katika kudai Katiba Mpya kwa kuwa, Rais Samia Suluhu Hassan, ana nia njema katika kufanya mabadiliko ya nchi.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima akiwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Migogoro ndoa, familia yashika kasi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwapo kwa ongezeko la mashauri ya migogoro ya ndoa na familia kwa asilimia 8.3 ndani miezi 11.

Akiwasilisha bungeni jana utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/24 na makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2024/25, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alisema hadi kufikia Aprili, mwaka huu, mashauri yaliyoshughulikiwa yalikuwa 31,380 ikilinganishwa na 28,773 yaliyoshughulikiwa mwaka 2022/23 ambayo ni ongezeko la mashauri 2,607 sawa na asilimia 8.3.

Alitoa wito kwa viongozi wa dini zote kuendelea kutoa mafunzo kwa wanandoa wanaofunga ndoa na kwa vijana kupitia mikusanyiko ya vijana katika madhehebu yao, ili kuwaandaa kubeba majukumu ya ndoa na kujiandaa kwa majukumu hayo kabla ya kuingia katika ndoa.

"Utulivu wa ndoa na familia ni msingi mkubwa ustawi wa familia na jamii kwa ujumla, kwani huzuia athari nyingi zikiwemo ukatili, Watoto wa mtaani na kuvunjika kwa ndoa," alisema.

Aidha, Dk. Gwajima alisema takwimu za Hali ya Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria Tanzania za mwaka 2022/2023 zinaonesha kupungua kwa vitendo vya ukeketaji nchini kutoka asilimia 10 kwa mwaka 2015/2016 hadi asilimia 8 kwa mwaka 2022/2023.

**WATOTO MITAANI WAONGEZEKA**

Dk. Gwajima alisema katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, mwakahuu, wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imepanua wigo wa utambuzi wa watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani kwa kuyafikia maeneo mengi zaidi ambayo ni masoko, vituo vya mabasi, minada na maeneo mengine yenye mikusanyiko ya shughuli za kiuchumi.

Alisema utambuzi huu, umewezesha kupata jumla ya watoto 8,372 wakiume 4,218 na wa kike 4,154 kutoka katika halmashauri za mikoa yote.

Aidha, katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili 2023, watoto waliotambuliwa walikuwa 5,728 wakiwamo wa kiume 4,583 na wa kike 1,145), sawa na ongezeko la watoto 2,644.

"Takwimu hizi zinaonyesha ukubwa wa tatizo la Watoto wa mtaani kuwa linaendelea kuongezeka," alisema.

Hata hivyo, alisema serikali bado imeendelea kuwapatia watoto hawa huduma zikiwemo kuunganishwa na familia zao (2,457), kuwawezesha kujitegemea katika jamii (873) na 5,042 wanaendelea kupatiwa huduma kwenye Makao ya Kulelea Watoto nchini kote.

Alifafanua kuwa sababu kubwa zinazochangia ongezeko hilo ni pamoja na hali duni ya maisha katika baadhi ya familia wanazotoka watoto hawa, msongo rika, malezi duni, pamoja na kuvunjika kwa ndoa.

Alitaja sababu nyingine ni pamoja na vifo vya mzazi/wazazi, au mlezi/tegemezi mkuu katika familia na kukosekana mbadala wa kuwalea watoto.

Alisema juhudi za pamoja zinahitajika katika kukabiliana na suala hili kuanzia ngazi ya familia, Mtaa au Kijiji, Kata, Wilaya, Mkoa kwa kushirikisha viongozi wa ngazi zote.

**VITAMBULISHO WAZEE**

Waziri huyo alisema hadi kufikia Aprili 2024, wazee 574,321 wanaume 214,739 na wanawake 359,582, wakiwamo wazee wasiojiweza 365,284 (wanaume 145,829 na wanawake 219,455) sawa na asilimia 63.6 ya wazee wote, waliofanyiwa tathmini, wamepatiwa vitambulisho maalum kwa ajili ya msamaha wa matibabu.

Dk. Gwajima alisema wizara iko katika hatua za mwisho za kukamilisha mabadiliko ya sera ya wazee ambayo miongoni mwa maboresho yatakayozingatiwa ni pamoja na umuhimu wa jamii kujiandaa kabla ya uzee.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Klabu Ligi Kuu msipuuze mashindano ya U-17, U-20

**WACHEZAJI** wenye viwango bora ni wale ambao wameandaliwa kuanzia ngazi ya chini na katika michezo ni nyota walioshiriki mashindano au ligi mbalimbali zinazohusisha vijana.

Mashindano hayo kwa hapa nchini si mengine bali ni Ligi ya Vijana ya umri chini ya miaka 17 na Ligi ya Vijana ya umri chini ya miaka 20.

Lakini kwa nchi zilizoendelea, wachezaji wenye umri chini ya hapo wamekuwa wakishiriki ligi maalum za watoto na wengi wao wakilelewa katika vituo vya michezo maarufu Akademi ambazo zinasimamiwa na makocha wenye elimu ya kufundisha mbinu za awali.

Na katika kuonyesha soka la vijana ndio litakalosaidia nchi au klabu kupata wachezaji bora watakaosaidia kuwapa matokeo ya ushindi, Shirikisho la Soka Afrika (CAF), limetambulisha michuano yake rasmi inayoshirikisha yosso wenye umri chini ya miaka 15.

Mashindano hayo yanayoitwa CAF African Schools Football Championship, mwaka huu yakiwa katika msimu wa pili na yanatarajia kufanyika kuanzia Mei 21 hadi 24 huko Zanzibar, yanashirikisha wachezaji wasichana na wavulana yakiwa na lengo la kuwaandaa na soka la ushindani.

CAF inaamini mataifa na klabu mbalimbali za Ulaya zinafanya vizuri katika mashindano wanayoshiriki, sababu kubwa ikiwa ni wachezaji wake waliandaliwa katika misingi sahihi, misingi hiyo ni kuwapa fursa ya kujifunza mchezo huo wakiwa na umri mdogo.

Hata hivyo bado kumekuwa na viashiria vya mataifa ya Afrika kupeleka wachezaji wenye umri mkubwa katika michuano hiyo ya U-15, jambo ambalo linawanyima wachezaji sahihi wanaotakiwa kuipata fursa hiyo muhimu.

CAF ikiwa na malengo ya kuibua vipaji, lakini inahitaji kuona wachezaji hawa vijana wanayapa pia kipaumbele masomo yao, ndio sababu zawadi ya fedha (Dola za Marekani 300,000), inayotolewa kwa mshindi hupelekwa katika miradi ya maendeleo ya kituo au nchi husika iliyoibuka kidedea.

Lakini kama nchi zitaendelea kudanganya umri wa wachezaji, hazitawaumia CAF na badala yake itapoteza nguvu kwa kuwapa nafasi wachezaji ambao hawatatumika kwa umri mrefu, kwa sababu watastaafu mapema kutokana na uhalisia wa viungo vyao kuanza kukataa kwenda na kasi ya mpira.

Hapa nyumbani katika jiji la Dar es Salaam kuna mashindano ya Ligi ya U-17 na U-20 yanaendelea katika viwanja vya TFF Kigamboni na Azam Complex huko Chamazi, lakini cha kusikitisha hakuna mawakala au mashabiki wanaofuatilia ligi hizo.

Kuyatupia kisogo mashindano hayo ni sawa na 'kujitupa' kaburini sisi wenyewe, shabiki namba moja wa mtoto ni mzazi au mlezi wake, na mzazi huyo anaweza kuwa kocha, meneja au kiongozi wa klabu mojawapo ambaye kama atapata nafasi ya kushuhudia chipukizi wetu wakipambana, huenda atapata nyota wa kuwasajili kwa ajili ya klabu yake.


Tunawakumbusha wadau wote wa mpira, ili chipukizi huyu afanye vizuri anahitaji kupata sapoti kuanzia kwa watu wake wa karibu na hatimaye yosso hao watatimiza ndoto zao za kucheza soka la kimataifa pale watakapoonekana na mawakala kutoka ama ndani au nje ya Tanzania.

Wadau twendeni kushuhudia vipaji vinavyoonyesha na vijana wetu, tunatakiwa tuamini wachezaji wa kigeni tunaowaleta kutoka nje huenda wengine wakapatikana hapa hapa na hao watasaidia kuifanya Timu ya Taifa (Taifa Stars), kuwa imara kwa sababu ni wachezaji wazawa.

Wahenda wanasema samaki mkunje angali mbichi, basi ni vyema pia viongozi, makocha na wadau wote wa soka wakawa na tabia ya kuyapa kipaumbele mashindano ya vijana ambayo yatasaidia kubaini wachezaji wenye vipaji watakaowasajili na kuponyesha 'mamilioni' ya fedha yanayotolewa kwa nyota wa kigeni kwa malengo ya kuimarisha viokosi vyao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Wanaompinga Mo Dewji Simba wamedhamiria au wachochezi?

**MSIMU** huu Simba haijafanya vizuri zaidi katika msimu wake wa mashindano mbalimbali, ingawa imerudia tena rekodi yake ile ile ya kucheza robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kwa wiki kadhaa kumekuwa na baadhi ya watu walimponda Mwekezaji wa Simba, Mohamed Dewji 'Mo Dewji', wakidai uwekezaji wake ni wa mashaka na haukidhi viwango kutokana na kiasi kidogo cha fedha anachoweka ili kuendesha timu.

Watu hao wa kada mbalimbali, wanadai Mo Dewji amekuwa akitoa pesa 'kiduchu', ndiyo maana kwa misimu mitatu wachezaji wanaosajiliwa ni wa viwango vya chini.

Halafu nikasikia baadhi ya wachambuzi redioni, wakisema eti wamepata taarifa kuwa Mo Dewji kwa sasa hatoi pesa, badala yake timu inajiendeesha kwa mapato ya klabu, yaani majengo yaliyopo Msimbazi, jezi, na vitu vingine vinavyofanana na hivyo.

Wanaosema hayo wakaenda mbali zaidi na kumtaka aondoke kwa sababu kuna matajiri wengi wanaitaka Simba ili waingize pesa nyingi kuliko ambazo yeye amekuwa akitoa.

Sipingi, kila mmoja ana haki ya kutoa mawazo au maoni yake, lakini haya wanayosemwa na hawa watu wanaoonekana kuionea huruma klabu hiyo kwa kufanya vibaya ni lazima yachambuliwe ili kuona kuna ukweli kiasi gani.

Tuanze na hili la Mo, ameitelekeza Simba na klabu imekuwa ikitumia mapato yake, ndiyo maana inasuasua katika mashindano na imeshindwa kusajili wachezaji bora.

Mimi nashindwa kuamini hili kwa sababu ziafuatazo. Klabu ya Simba imekuwa ikisafiri ndani na nje ya nchi kwa kutumia ndege. Imecheza mechi zote za Ligi ya Mabingwa, ikisafiri na wachezaji, makocha, viongozi na watu waliohitajika na kwenda kukaa kwenye hoteli kubwa mpaka ilipotolewa hatua ya robo fainali.

Katika mechi za Ligi Kuu, imekuwa ikisafiri kwa ndege na kukaa kwenye hoteli za nyota tano kote huko. Hivi tuamini kweli hizi ni pesa za mapato ya klabu? Kwa wale mashabiki wa soka wa miaka mingi nyuma kabla ya Mo, wanakumbuka jinsi timu ilivyokuwa ikienda kucheza mechi za ligi mikoani kwa kutumia usafiri wa basi. Ikisafiri kwa ndege labda nje ya nchi. Pesa za mapato ya klabu hazikuwepo?

Leo hii hatujawahi kusikia wachezaji na wafanyakazi wote wa Simba hawajalipwa mishahara, pia huyo huyo mwekezaji ndiye anawajibika kusajili na kuzitunza timu za wanawake, Simba Queens, ile ya chini ya miaka 20 na 17 ambazo zinafanya vizuri sana kwenye michuano mbalimbali inayoshiriki, wala hatujasikia matatizo yoyote, ikiwemo kucheleweshewa mishahara, posho, au kutosafiri kwa sababu pesa hakuna.

Lingetokea hili, hata mimi ningeamini upande wa mwekezaji kuna matatizo. Sehemu pekee ambayo inaonekana ina matatizo Simba ni kwenye usajili tu wa wachezaji wa timu kubwa.

Kama kila kitu kinapatikana, lakini tatizo lipo kwenye kusajili wachezaji wasio na viwango, hilo nadhani sasa siyo kosa la mwekezaji, bali ni viongozi waliopewa dhamana. Nadhani ndiyo wanaomwangusha mwekezaji kwenye eneo hili na kupokea ukosoaji mkubwa kutoka kwa baadhi ya watu. Mo hawezi kuchukua pesa yake na kuanza kupita huku na huko kusaka wachezaji.

Hii ni sawa na baba nyumbani hawezi kutoa pesa ya chakula na kuanza kufuatilia mama amepika chakula gani, je kina thamani ya ile pesa ambayo ametoa? Huyo mwanaume ataambiwa ana hila. Uaminifu unatakiwa uwe kwa aliyepewa dhamana hiyo.

Ni kukosa shukrani kwa mwekezaji huyo ambaye uwekezaji wake umeifanya Simba kuwa moja kati ya klabu zilizo ndani ya 10 bora barani Afrika kwa sasa, na maarufu zaidi. Ndiye aliyeifanya Simba kucheza robo fainali ya Ligi ya Mabingwa iwe ni kawaida kwa sasa kiasi cha Tanzania kuanza kupeleka timu nne, badala ya mbili. Huu ni ukweli mtamu na mchungu pia.

Nadhani wanaoongea hivyo wanafanya makusudi labda ili asuse, aondoke, halafu iwe faida kwa klabu zingine, au tayari yupo mwekezaji ambaye anaitaka klabu, lakini anapitia mlango wa nyuma kwa ajili ya kumtia hasira kumwambia hajafanya kitu ili aondoke.

Vinginevyo ni kupata matajiri kwenye soka ni ngumu sana, hakuna mwenye pesa ambaye anaingiza kwenye mpira halafu kila kukicha anasemwa vibaya.

# Njombe wafurahia msukumo wa Rais Liganga na Mchuchuma

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

SERIKALI mkoani Njombe imesema kuwapo kwa msukumo wa Rais Samia Suluhu Hassan wa kuziagiza Wizara ya Viwanda na Biashara na Ofisi ya Rais Mipango nas Uwekezaji kuhusu miradi ya Mchuchuma na Liganga, ni fursa tosha kwa maendeleo ya mkoa na taifa kwa ujumla.

Rais Samia hivi karibuni aliagiza wizara hizo kutafuta kampuni itakayochimba madini ya chuma Liganga na makaa ya mawe Mchuchuma wilayani hapa ili kuacha kuagiza malighafi hiyo kutoka nje ya nchi.

Pia imesema kuanza kwa mradi huo ni mapinduzi makubwa ya kiuchumi yanatajwa sambamba na kukuza pato la taifa na kuondokana na ukosefu wa ajira kwa Watanzania.

Akizungumza juzi katika eneo la madini ya chuma Liganga, Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, alisema Rais Samia amesema anatamani kuona mradi wa Liganga na Mchuchuma unaanza mara moja.

"Matarajio yetu ni kwamba tukitekeleza mradi huu, dunia iko kwenye mapinduzi ya nne ya viwanda. Hapa Tanzania tunatekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa reli ya kisasa na tunaenda kwenye awamu nyingine ya ujenzi wa reli ya Zambia kuja Tanzania.

"Pengine tunapoenda mradi huu ukiwa umefanya kazi hata mataluma ya reli yatatoka kwenye mradi huu," alisema.

Mtaka alibainisha kuwa mkoa umeipa thamani wilaya ya Ludewa kwa kuamua kujengwa chuo cha mafunzo ya ufundi stadi (VETA) katika kijiji cha shaurimoyo badala ya kujengwa makao makuu, Njombe mjini.

Naye Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Judica Omari, aliwataka wananchi kuwekeza katika maeneo jirani na mradi huo ili kuhakikisha wawekezaji wanapokuja wanapata maeneo ya kulala na kilimo.

Diwani wa Mundindi, Wice Mgina, alisema wananchi tayari wamelipwa fidia na wamefanya vitu ambavyo vitasaidia kukuza vipato vyao na familia kwa ujumla.

Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Njombe, Mhandisi Ruth Shalua, alisema wanajenga barabara za zege ili kujiandaa kwa kuanza mradi huo wa kimkakati ili barabara ziwe na uimara wa kutosha kubeba hii malighafi ya chuma pamoja na makaa ya mawe kwenda viwandani.

Mmoja wa wakazi walioko jirani na mradi wa Liganga, Ibrahim Mkinga, alisema wameanza kuchangamkia fursa mbalimbali ikiwamo ujenzi wa hoteli.

"Furaha yangu kubwa ambayo ninaitegemea kwamba chuma kikianza tayari nimewekeza ujenzi wa jengo hili na faida ya kwanza nitapata wageni ambao watasaidia uchumi wangu kupanda zaidi," alisema Mkinga.



Sehemu ya Barabara ya Mtaa wa Kalenga, Upanga Magharibi, jijini Dar es Salaam, ikiwa imeanza kujengwa kwa kiwango cha zege jana, kutokana na kuharibika mara kwa mara hasa nyakati za mvua. **PICHA: JOHN BADI**

# Vijana 490 waokolewa kutoka mazingira hatarishi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

VIJANA 490 wenye umri kati ya miaka 14 na 24, wakiwamo mabinti waliopata watoto wakiwa katika umri mdogo, Kilosa mkoani Morogoro, wameokolewa kutoka kwenye mazingira magumu waliyokuwa wakiishi na kujihusisha na biashara haramu ya kuuza miili ili kujipatia riziki.

Vijana hao wamewezeshwa kwa mafunzo mbalimbali ya biashara na ujasiriamali ili kujipatia kipato halali.

Mabinti hao wameokolewa kupitia mradi wa kuboresha fursa za vijana wa Kitanzania kujiajiri ili kuepukana na umasikini (SET) unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Uswisi kupitia ubalozi wa nchi hiyo Tanzania.

Mradi huo unaotekelezwa na Shirika la Swisscontact Tanzania kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali nchini, umewapatia mafunzo vijana hao ya yakiwamo ya ushonaji na uanzishaji wa biashara, uchakataji wa vyakula, usindikaji wa maziwa na masuala ya jinsia.

Mwenyekiti wa kikundi cha vijana hao cha Upendo kilichoko kata ya Ulaya wilayani Kilosa, Tausi Lyadiga, alisema kabla ya mafunzo hayo, baadhi yao walikuwa wakitegemea kujipatia kipato kwa kulaghaiwa na wanaume kufanya ngono.

"Una mtoto mdogo, anahitaji kula na hela huna. Mwanamume aliyekuzalisha ndiyo kama hivyo amekutelekeza, basi unajikuta unarubunika kwa wanaume wengine ili kujipatia kipato na anaweza kukupatia Sh. 2,000 mpaka 5,000," alisema.

Lyadiga alisema baada ya mafunzo hayo, wameanzisha kikundi chenye watu 25 cha kusindika na kutengeneza maziwa ya mgando, viazi vilivyosindikwa na kutoa huduma ya vyakula kwenye shughuli mbalimbali, hivyo kuwawezesha kujipatia kipato halali.

Alisema licha ya kuwamo katika kikundi hicho, ameangalia fursa zaidi kwa kufanya biashara ya mitumba na kumwezesha kujipatia kipato hatimaye kusomesha mtoto wake, kusaidia familia na kununua kiwanja ambacho anatarajia kuanza ujenzi wa nyumba yake.

**Vijana hao wamewezeshwa kwa mafunzo mbalimbali ya biashara na ujasiriamali ili kujipatia kipato halali.**

"Kwa kweli nawashukuru sana Swisscotact kupitia mradi wa SET kwa mafunzo. Hivi sasa hakuna mwanamume anayenibabaisha kwa hela zake. Mimi mwenyewe nafanya biashara ya nguo, napata hela, nasomemesha mtoto wangu. Pia nawasaidia wazazi na wadogo zangu lakini kwa sasa ninaanza ujenzi wa nyumba yangu wakati wowote," alisema.

Naye Pili Simba, mkazi wa kijiji cha Ulaya ambaye ni mnufaika wa mafunzo hayo, alisema yamemsaidia kuanzisha saluni ya kike ambaye kwa siku inamwingizia kati ya sh 15,000 na 50,000 kulingana na misimu ya kilimo kitu ambacho kinamwezesha kumudu maisha na kuondokana na utegemezi kutoka kwa wazazi.

"Mimi nina mtoto, hivyo biashara ya saluni inanipa kipato kikubwa. Naweza kujimudu kimaisha na pia nafanya shughuli za kilimo cha mpunga na ufuta navyo vinanilipa. Napata fedha za kutosha," alisema.

Mnufaika mwingine, Zuena Yassin, alisema baada ya mafunzo hayo na kushiriki katika kikundi, alimua kujiongeza na kujifundisha cherehani na baadaye alimua kununua cherehani yake na kuanza kushona nguo huku akifanya biashara nyingine kwa kufungua mgahawa wa kuuza vyakula mbalimbali.

Ofisa Mawasiliano na Habari wa Swiscontact, Mafunga Isumbi, alisema mradi wa SET umenufaisha vijana 559 wakiwamo wa kiume 69 na wa kike 490 katika kata za Berega, Chanzuru, Msowero, Mtumbatu, Mvumi, Rudewa na Ulaya kupitia taasisi za MVIWAMORO, CSCA na CRESD ambazo zilipewa kazi ya kutoa mafunzo hayo.

Alisema mradi huo umelenga kusaidia vijana wa kiume na wa kike ambao zaidi wa kike waliopata watoto wakiwa bado wadogo ambao wawanalea bila kuwa na usaidizi baada ya kutelekezwa na wenzi wao.

# Tanzania, Canada kuimarisha ushirikiano kwa manufaa zaidi

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amekutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Maendeleo ya Kimataifa wa Canada, Ahmed Hussein, Ikulu jijini Dar es Salaam.

Katika mazungumzo hayo juzi, Dk. Mpango alisema Tanzania inathamini uhusiano wa kidiplomasia uliopo baina yake na Canada na kuishukuru kwa kuiunga mkono Tanzania katika sekta mbalimbali zikiwamo afya, elimu, biashara na uwekezaji, kilimo, ulinzi na usalama.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ofisi ya makamu wa Rais, Dk,. Mpango alisema mataifa haya mawili yameendelea kushirikiana kimataifa ikiwamo Jumuiya ya Madola na Umoja wa Mataifa.

Makamu wa Rais aliikaribisha Canada kushirikiana na Tanzania katika kuimarisha uchumi wa buluu kwa kutumia uzoefu wa nchi hiyo pamoja na kukaribisha wawekezaji katika sekta hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Makamu wa Rais pia aliishukuru serikali ya Canada kwa kuunga mkono ajenda ya Rais Samia Suluhu Hassan ya nishati safi ya kupikia.

Alisema kuunga mkono jitihada hizo kutaharakisha wananchi wa Tanzania kuondokana na nishati isiyofaa ya kupikia na kufikia malengo ya mkakati wa kitaifa wa kufikia asilimia 80 ya matumizi ya nishati safi ifikapo mwaka 2034.

Dk. Mpango alisema kwa sasa Tanzania ni sehemu sahihi zaidi kuwekeza kwa kuwa serikali imewekeza katika kuimarisha uchumi na kuweka mazingira mazuri zaidi ya uwekezaji na biashara kwa kufanya mageuzi ya kitaasisi, kisera na kuimarisha utawala wa demokrasia.

Pia amesema ni muhimu kufanya kazi pamoja katika kuharakisha majadiliano ya kuboresha mkataba wenye usawa na maslahi kwa pande zote mbili wa kinga katika uwekezaji baina ya Canada na Tanzania (FIPA).

Aidha, alisema serikali ya Canada inaweza kushirikiana zaidi na Tanzania katika sekta ya afya kwa ujenzi wa viwanda vya kuzalisha dawa, kuwekeza katika makao makuu ya nchi Dodoma katika ujenzi wa miundombinu, udhibiti wa taka ngumu, viwanja vya michezo na mazao ya mboga.

Makamu wa Rais aliishukuru serikali ya Canada kwa kuiunga mkono Tanzania dozi milioni 22 za vitamini A pamoja na kutangaza ahadi ya dola milioni 25 katika mradi wa kilimo rafiki kwa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Naye Waziri Hussen alisema uhusiano wa Tanzania na Canada ni wa muda mrefu katika hali zote ambao umeendelea kuimarika.

Alisema katika wakati huu ambao Tanzania imefikia uchumi wa kati wa chini, ni muda mwafaka wa kuongeza ushirikiano baina ya mataifa hayo mawili.

Hussein alisema katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi, Canada inatambua umuhimu wa kufanya kazi pamoja ili kuondoa athari kwa wananchi.

Waziri huyo alitoa pole kwa serikali na wananchi wa Tanzania na familia zilizoathirika na kimbunga hidaya pamoja na mvua za el nino zilizopelekea madhara makubwa.

Aliongeza kwamba Canada inaendesha miradi mbalimbali Tanzania ikiwamo ya kuwajengea uwezo wananchi katika kuhimili mabadiliko ya tabianchi pamoja na kilimo rafiki kwa mazingira.

Waziri Hussen pia alisema Canada itaendelea kushirikiana na Tanzania katika sekta mbalimbali zikiwamo mazingira, afya, lishe na elimu.



Mchuuzi wa mananasi akisubiri wateja kando ya Barabara ya Sam Nujoma, eneo la Mwenge Mpakani, Manispaa ya Kinondoni Dar es Salaam juzi. Ukosefu wa masoko ya kutosha umekuwa ukisababisha baadhi yao kufanya biashara katika maeneo yasiyo rasmi. **PICHA: SABATO KASIKA**

## DC awatumia salamu wazembe, wabadhirifu

**Na Steven William** MUHEZA

MKUU wa Wilaya ya Muheza, Zainab Abdallah, ameonya kuwa hatamwonea huruma mtumishi yeyote atakaechezea fedha za serikali au kuzembea kutekeleza miradi kwa wakati.

Alitoa onyo hilo juzi katika kikao kazi na watumishi wote kujadili miradi inayotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kwa miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan ambacho kilimalizika saa 4:30 usiku.

Mkuu huyo wa wilaya alisema wale wote watakaobainika kuhujumu miradi ndani ya miaka mitatu hii ya Rais Samia hata kama wamehama kituo cha kazi, watarudishwa na kuja kujibu hoja za serikali,

Alisema wamefanya kikao kazi cha kujadili miradi inayotekelezwa na halmashauri na kwamba wameweka mikakati na maazimio ambayo yatakuwa mwarobaini wa changamoto katika wilaya.

Zainab alisema moja ya mikakati hiyo ni kupambana na tabia ya kutokukamilisha miradi kwa wakati, miradi kuwa chini ya viwango, fedha kuisha na miradi kutokukamilika, fedha za miradi kukaa muda mrefu kwenye akauniti bila kutumika na changamoto nyingi zilizobainika na kusababisha miradi kutokukamilika.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Muheza, Mohamed Mfaki, alisema kazi iliyobaki hivi sasa ni kuhakikisha miradi ya maendeleo inasimamiwa na kukamilika kwa haraka pamoja na kusimamia vizuri matumizi ya fedha za serikali.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, dk. Jumaa Mhina, alisema kwa kushirikiana na timu yake ya watumishi, amepokea maagizo hayo na kwamba anamshukuru Rais Samia kwa kutoa fedha nyingi za miradi ya maendeleo wilayani hapa.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Erasto Mhina, alisema kwa niaba ya madiwani wenzake, wamejipanga kusimamia miradi katika kata zao ili kukamilika kwa wakati na kuhakikisha fedha za serikali zinatumika vizuri.

# Huduma wagonjwa hospitali rufani kidijitali

**Na Pilly Kigome**

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa ya Amana, inajipanga kuanza kutoa huduma za matibabu kwa wagonjwa kupitia mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kabla ya kufika hospitalini hapo.

Lengo la kufanya hivyo ni kupunguza msongamano, kurahisisha na kuboresha huduma zake.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. John Kingu, alisema juzi jijini Dar es Salaam kuwa katika kuboresha huduma kwenye hospitali za rufani nchini, serikali imeagiza kuboresha zaidi huduma kwa wananchi ikiwamo matumizi ya TEHAMA.

Alisema wagonjwa wanatakiwa watumie mifumo ya kuweka miadi kabla ya kufika kupatiwa matibabu na kupangiwa siku na muda wa kumwona daktari husika na kupatiwa matibabu. Alisema hatua hiyo itasaidia na kurahisisha kuimarisha kutoa huduma kwa wagonjwa.

"Teknolojia hii itarahisisha huduma na kuondoa tatizo la wagonjwa kupoteza muda wa kukaa hospitalini kwa kipindi kirefu na baadaye kukosa muda wa kutibiwa. Pia itawaepusha wagonjwa kuamka usiku wa manane kuwahi foleni za matibabu.

"Mtu kokote aliko awe anatoka Dar es Salaam au mkoaani, atapiga simu au kutumia mifumo ya barua pepe na mingine itakayowekwa kuomba kufika hospitalini kutibiwa bila kujali simu ni ya kisasa au kitochi, mfumo huo utawafikia," alisema.

Katika hatua nyingine, Dk. Kingu aliikabidhi hati ya umiliki wa ardhi hospitali hiyo yenye ukubwa wa ekari sita. Awali hospitali hiyo ilikuwa inaendesha shughuli zake bila kuwa na hatimiliki.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Amana, Dk. Bryceson Kiwelu, alisema wamelipokea agizo la katibu mkuu kwa kuwa walikuwa wanakabiliwa na msongamano na malamamiko mengi kutoka kwa wagonjwa kutokana na kila mmoja kutaka kutibiwa kwa wakati.

Alisema wanajipanga kuanza kutoa elimu kwa wananchi na wagonjwa kuhusiana na matumizi ya teknolojia ya kutumia mifumo hiyo kabla ya kuanza kutumia rasmi ili kuondoa sintofahamu kwa wagonjwa.

Dk. Kiwelu alisema mfumo wa TEHAMA ulianza mwaka 2012 kwa kuwahudumia wagonjwa kwa kupatiwa majibu na huduma zingine lakini bila kutumia kwa kufanya miada kufika hapo. Alisema huduma hiyo mpya itaanza muda wowote kuanzia sasa.

"Mfumo huu utatusaidia kwa kiwango kikubwa kwani kinachotokea sasa hivi wagonjwa wote wanafika kwa wakati mmoja na kila mmoja anaona muhimu kupatiwa huduma kuliko mwingine," alisema Dk. Kiwelu.

Alisema wastani wa kupokea wagonjwa hospitalini hapo ni wagonjwa 650 hadi 700 kwa siku na kwamba idadi imepungua tangu kutokea kwa janga la UVIKO-19. Alisema awali walikuwa wakipokea wagonjwa 1000 au zaidi.



## RAS akemea malezi watoto kama mayai

Na Thobias Mwanakatwe, MKALAMA

KATIBU Tawala Mkoa wa Singida Dk. Fatuma Mganga, amewataka wazazi kuacha kuwalea watoto wao kama mayai badala yake watimize wajibu wao kila mmoja katika familia ili kuwa na jamii bora kwa maendeleo bora ya Taifa.

Alisema hayo jana wakati wa kongamano la Siku ya Familia Duniani lililofanyika kimkoa katika kata ya Ibaga wilayani hapa na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali, vyama vya siasa, dini pamoja na wananchi.

"Kila mmoja atimize wajibu wake. Tusaidiane, tushirikiane kulea familia vizuri lakini pia tusilee watoto wetu kama mayai. Tufuatilie mienendo ya watoto wetu, suala la kutengeneza familia bora si suala la Serikali, ni suala la kila familia. Wazazi tutimize wajibu wetu tusiwachekee watoto wetu," alisema.

Dk. Mganga alisema baba ni kichwa cha familia, hivyo wanalo jukumu kubwa la kusimamia familia kikamilifu kwa kuchukua nafasi zao katika familia ili kuiwezesha familia kuwa na bora na ya kuigwa ndani ya jamii.

Awali, akiwasilisha hoja kuhusu chanzo cha familia nyingi kuvunjika, Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, Moses Machali, alisema kukosekana kwa uwazi baina ya wana ndoa kunapelekea ndoa nyingi kuwa na migogoro.

Alisema suala la ushirikishwaji katika familia ni muhimu kwakuwa panapokosekana ushirikishwaji kunaleta migogoro ambayo inapelekea familia kutengana hivyo amewasihi wanafamilia kuwa na tabia na maadili mema sambamba kwa kufanya kazi kwa bidii ili kujiongezea kipato na kumudu mahitaji ya familia.

"Kama ni kulima, baba lima sana kama ni mama fanya kazi za kuongeza kipato cha famili, kazi ya kutunza familia ni jukumu letu sote," alisema.

# Mufti akabidhi mkakati kudhibiti uvunjifu maadili, migogoro ya ndoa

Na Peter Mkwavila, DODOMA

SHEIKH Mkuu wa Tanzania, Mufti Abubakar Zuberi, amekabidhi mpango mkakati wa mmonyoko wa maadili kwa viongozi wa dini ya Kiislamu mkoani Dodoma unaolenga kunusuru wimbi la kuvunjika kwa ndoa.

Akizungumza jana baada ya kukabidhi mpango huo kwa Sheikh wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, kwa niaba ya viongozi hao, Mufti Zuberi alisema bado kwenye jamii kuna ukosefu wa elimu ya malezi ya kulinda ndoa hali ambayo imesababisha kuwapo kwa talaka nyingi.

Alisema kuwa kupatikana kwa mwongozo huo dini hiyo kutasaidia kuzuia uvunjikaji wa ndoa na wingi wa watoto wasiokuwa na malezi ya pande zote mbili.

Naye Naibu Kadhi Mkuu wa Tanzania, Sheikh Ally Ngeruko, alisema mpango huo unalenga kulinda misingi ya dini, kuimarisha umoja na amani, kuendeleza nidhamu na heshima na kukuza malezi bora.

Pia alisema misingi mingine ni pamoja na kuinua ubora wa ibada, kupunguza migogoro na mzozo,kuimarisha uwajibikaji,kuchochea maendeleo ya jamii,kulinda sifa ya dini na msikiti na kujenga msingi wa jamii thabiti.

Sheikh Ngeruko alisema lengo kuu ni kuunda mpango huo ni kutoa elimu ya kisheria,kupunguza mmmonyoko wa maadili,kuimarisha usuluhishi na upatanishi,kukuza ushirikiano na madrasa.

Pia alisema mpango huo unalenga kutoa mwongozo wa maadili, kuwajengea uwezo viongozi wa kata, kutoa mafunzo kwa viongozi wa dini,kusimamia semina na kozi kuunda jamii yenye maadili thabiti.

Naibu Kadhi huyo alisema zaidi ya asilimia 70 ya wanandoa walio wengi wamekosa elimu kuhusu ndoa hali ambayo imekuwa ikisababisha migogoro na kupeana talaka na baadhi ya watoto kukosa malezi ya pande zote mbili.

Awali, Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Sheikh Khamis Mataka, alisema: "Talaka zimekuwa kama njugu, kila mmoja analalamika kuhusu masuala ya maadili BAKWATA tumeona tunatakiwa kufanya jambo juu ya jambo hilo."

Sheikh wa Mkoa wa Dodoma, Rajabu, alisema wamepokea miongozo hiyo na wataifanyia kazi na kwamba itakabidhiwa kwa Mashehe,maimamu walimu wa madrasa pamoja na wakuu wa idara ya wanawake na vijana.

"Viongozi wangu nami nimeanza kazi hapa hapa miongozo hii nitaikabidhi kwa viongozi wangu wote kuanzia hivi sasa kinachofuata ni utekelezaji tu ambao kila kiongozi anatakiwa kuwa balozi wa kuelimisha kuhusu huu mpango mkakati wa idara ya elimu katika ofisi yetu ya mahakama ya kadhi ili kudhibiti mmomonyoko wa maadili," alisema.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama (kushoto), akijadiliana jambo na Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na wenye Ulemavu, Deogratius Ndejembi, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mfumo kuwapunguzia majaji mzigo waanza

Na Renatha Msungu, DODOMA

MAHAKAMA 11 nchini zimeanza kutumia mfumo wa kutafsiri unaojulikana kama 'Transcription and Translation Software' (TTS), unaolenga kuwapunguzia majaji na mahakimu mzigo wa kuandika mienendo ya mashauri kwa mkono.

Jaji Kiongozi Mustapha Siyani alibainisha hayo jana alipokuwa akifungua Baraza la Wafanyakazi wa Mahakama kwa niaba ya Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, jijini hapa.

Alisema mfumo huo umefungwa baadhi ya Mahakama Kuu ambazo pia ni masjala ndogo za Mahakama ya Rufani.

"Nirudie kusisitiza kuwa mfumo huu wa TTS utaongeza ufanisi katika uchukuaji wa mwenendo wa shauri kwa kumpunguzia Jaji/Hakimu mzigo wa kusikiliza na kuandika kwa wakati mmoja, na kuharakisha kupatikana kwa mienendo ya mashauri kwa ajili ya kukata rufani,"alisema.

Aidha, alisema mfumo mpya wa usimamizi wa mashauri (e-CMS), utaondoa malalamiko ya watumishi wa mahakama kupokea rushwa ili watoe huduma.

Jaji huyo aliiomba Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU) kuisaidia Mahakama kufanya tathmini ya mitazamo, hisia na dhana za rushwa kutoka kwa wananchi dhidi ya mhimili huo.

"Mahakama imekuja na mifumo ya kidijitali ambayo licha ya kuondoa dhana hii itarahisisha kazi kwa majaji na mahakimu nchini,"alisema.

Alisema mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) inayotumiwa na Mahakama ya inawalenga wananchi na watumiaji wa huduma za Mahakama kwa kuwapa huduma kwa weledi, ufanisi, uwazi na kwa haraka.

Mfumo huo, pia alisema utasaidia kupima utendaji wa kila mmoja wetu bila ubaguzi au uonevu kwa watumishi na kuongeza tija, ufanisi na uono wa viwango vya utoaji wa huduma wa kila mtumiaji wa mfumo huo.

Alisema watumishi watapunguza kukutana na wadau uso kwa uso na kuondoa lawama za kimaadili kwa vile wadau na wananchi watapata fursa ya kuingia katika mfumo kutafuta taarifa bila kumuona mtumishi wa Mahakama.

Naye Katibu Msaidizi wa Baraza la Wafanyakazi wa Mahakama, Christina Edward, ambaye ni Hakimu Mkazi alisema mkutano huo utakwenda kubadilisha utendaji wa kazi zao kutokana na changamoto watakazojadili.

Alisema watatekeleza maagizo yote yaliyotolewa ili kuhakikisha wanakwenda kufanya kazi kwa ufanisi ikiwamo kutumia mfumo huo.

Hata hivyo, aliwataka watumishi wa mahakama kila mmoja kuzingatia yale yanayotolewa ili kwenda kuwapa elimu na watumishi ambao hawakubahatika kuhudhuria Baraza hilo.





# SMZ yajizatiti mapambano mabadiliko tabianchi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JITIHADA za pamoja zinahitajika katika upandaji na utunzaji wa miti ili kuirejesha Zanzibar ya Kijani kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Upandaji wa miti ni fursa adhimu ambayo ikitumika vyema inaweza kutunufaisha kwa kurejesha uoto wa asili uliopotea pamoja na manufaa yatokanayo na biashara yakaboni.

Akiwasilisha makadirio ya matumizi na mapato ya wizara yake, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Haruos Suleiman Said, alisema serikali imejipanga katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi yanayotokana na athari kubwa za mazingira.

Alisema Zanzibar inatekeleza mradi wa uhimili mabadiliko ya tabia ya nchi kwa jamii za pwani ambazo kwa kiasi kikubwa zimeathirika kutokana na kasi ya maji ya bahari kujaa juu na kutishia maisha ya wananchi.

Alizitaja juhudi zinazochukuliwa kuwa ni Pamoja na wananchi wa Pemba katika shehia za Sipwese na Mkungu kujenga matuta mawili makubwa kuzuia maji ya bahari kuingia katika mashamba ya wakulima.

Waziri huyo alisema ukataji wa miti ya aina mbalimbali ikiwamo mikoko pembezoni mwa Bahari, umesababisha athari kubwa na ndiyo chanzo cha maji ya bahari kujaa na kuingia katika maeneo ya makazi.

"Tunawataka wananchi na kinamama kwa ujumla sasa kuachana na ukataji wa kuni kwa ajili ya kupikia. Mwelekeo kwa sasa ni matumizi ya gesi sahihi kulinda mazingira," alisema.

Jumla ya Sh. 19,057,370,840 zimeidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2024/25 ambapo suala la kulinda na kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi limepewa kipaumbele.

# Mzigo UKIMWI waelemea zaidi wanawake

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

OFISI ya Makamu wa Kwanza wa Rais imesema UKIMWI unaendelea kuwaelemea zaidi wanawake kuliko wanaume visiwani hapa.

Kwa mujibu wa ofisi hiyo, kati ya watu 10,580 wanaokisiwa kuishi na virusi vya UKIMWI (VVU), wanawake ni 6,206 kUlinganisha na wanaume ambao ni 4,374.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harous Suleiman Said, alisema hayo jana wakati akiwasilisha makadirio yamapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka wa fedha 2024/25 katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani nje ya mji wa Zanzibar.

Alisema utafiti wa viashiria vya maambukizo ya VVU kwa mwaka 2023 umeonyesha kwamba asilimia 0.4 ya Wazanzibari wanaishi na VVU ikiwa ni sawa na watu 10,580.

Waziri alisema idadi hiyo si ndogo kulinganisha na watu Zanzibar na kwamba hadi kufikia Desemba 2023, watu 8,766 wanaoishi na VVU walikuwa wamesajiliwa na kuendelea kupata huduma katika vituo vya matibabu.

Alisema katika kuimarisha upatikanaji wa huduma za UKIMWI, ofisi yake imeendelea kuhamasisha jamii Unguja na Pemba kwa watunga sheria na wasimamizi wa sheria juu ya haki ya huduma za VVU kwa wanaoishi na virusi hivyo na makundi maalum ili wazielewe.

Alisema utafiti pia umeonesha kwamba asilimia 0.4 ya Wazanzibari wanaishi na VVU ambapo asilimia 0.5 Unguja na asilimia 0.3 Pemba.

Mkoa wa Kusini Unguja, alisema unaongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya watu wanaoishi na VVU ukiwa na asilimia 0.8 ukifuatiwa na askazini Unguja asilimia 0.7 na Kaskazini Pemba ndio wenye asilimia ndogo kabisa kwa kuwa na asilimia 0.2.

Pia alisema ofisi yake imeratibu shughuli za vituo vya tiba vya VVU na vituo vya huduma rafiki kwa vijana ili kuangalia huduma za VVU na afya ya uzazi.

Alisema hadi kufikia Februari, mwaka huu, kupitia vituo hivyo, watu 15,024 walipima VVU na 285 kati yao waligundulika na maambukizi.

Waziri huyo alisema wanawake wanaoishi na VVU 1,365 walifanyiwa uchunguzi wa saratani ya mlango wa shingo ya kizazi na 40 waligundulika na tatizo hilo katika kliniki za tiba.

"Watu 18,351 walifanyiwa uchunguzi wa magonjwa ya kujamiiana na 434 walikuwa wameambukizwa," alisema.

Hata hivyo, alisema ofisi yake imefanya uratibu wa Programu ya GREAT ambayo inalenga kumwezesha mtoto wa kike kuimarisha afya ya uzazi na kujikinga na maambukizo ya VVU inayotekelezwa na taasisi za serikali na asasi za kiraia.

Alisema takribani ya vijana 337,099 wamefikiwa kwa kupatiwa elimu, walimu 2,013, wahudumu wa afya wa kujitolea 1,438 na wahudumu wa afya wa vituoni 519 walipatiwa mafunzo kupitia programu hiyo.



Mafundi wa Kampuni ya Sinohydro, wakijenga chemba ya maji ya mvua katika barabara ya mabasi ya mwendokasi, eneo la Mbagala jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ofisi AG, India kushirikiana kwakunoa wataalamu

**Na Mwandishi Wetu**

OFISI ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar na Chuo Kikuu cha Taifa cha Sheria cha Jodhpur cha India (NLUJ) zimetia saini hati ya makubaliano ya ushirikiano kwa lengo la kujengeana uwezo katika tasnia ya sheria.

Makubaliano hayo yalitiwa saini jana na Naibu Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Shaaban Ramadhan Abdalla na Makamu Mkuu wa NLUJ, Prof. Harpreet Kaur katika ukumbi wa chuo hicho, Jimbo la Jodhpur, India.

Akizungumza baada ya kutiliana saini hati hiyo, Naibu Mwanasheria Mkuu alisema makubaliano hayo ni matokeo ya ziara yao ya mafunzo ya wiki mbili nchini India yalifadhiliwa na Serikali ya India (Wizara ya Mambo ya Nje) kupitia programu yao ya mpango wa ushirikiano wa kiufundi na kiuchumi wa India (ITEC)

Alisema makubaliano hayo yatatoa fursa kwa watendaji wa Afisi yake kuongeza maarifa na utaalamu katika maeneo mbali mbali ya fani zao kwa faida ya Serikali na wananchi kwa ujumla.

Alisema Chuo cha NLUJ ni chuo kilicholeta mapinduzi makubwa katika nyanja ya ufundishaji nchini India, hivyo ni wazi kuwa watendaji wataongeza ujuzi wao kutokana na kuweza kupata uzoefu mkubwa wa wataalam wa sheria wa Chuo hicho.

Naye Prof. Kaur alisema makubaliano hayo si tu yatakuza juhudi za kitaaluma kati ya Zanzibar na India, bali pia yatakuza urafiki na kubadilishana utamaduni wa nchi hizo.

Alisema kuwa makubaliano hayo pia yatazingatia namna na mbinu bora zaidi za kupeana maarifa pamoja na kuweza kufanya tafiti mbali mbali za kitaaluma kwa maslahi ya sekta ya sheria na maendeleo kwa ujumla wake. Aidha, alisema kupitia makubaliano hayo, fursa na utekelezaji wa programu za mafunzo ya kujengeana uwezo zitaendeshwa kwa mashirikiano ya pamoja ambazo zitakuwa zikifanywa kwa nadharia na vitendo yatakayoongozwa zaidi na matumizi ya teknolojia ya kisasa.

Prof. Kaur alisema mMakubaliano hayo pia yatatoa fursa kwa vitivo katika chuo hicho, wanafunzi, mawakili wa serikali, maafisa sheria na watafiti kutoka katika taasisi hizo mbili kufanya tafiti kuhusiana na mada mbalimbali zitakazoibuliwa kuhusiana na sheria kama vile usuluhishi na njia mbadala za utatuzi wa migogoro, uandishi wa sheria , mikataba, biashara, utumiaji wa akili bandia katika uandaaji wa hati za madai na uendeshaji wa mashauri, pamoja na kuzingatia masuala mengine yanayohusiana na utawala na uendeshaji wa taasisi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje ya NLUJ, Dk. Neeti Mathur, alisema ana matumaini makubwa kuwa kila upande utanufaika vyema na Makubaliano hayo yanayohusu taaluma na kujengeana uwezo katika mambo mbali mbali yenye mustakabali mzuri unaolenga ustawi wa tasisi zote mbili na maslahi mapana kitaifa.

Aidha Mkurugenzi wa Rasilimali Watu, Utawala na Mipango, Fatma Iddi Ally, alimshukuru Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Dk. Mwinyi Talib Haji, kwa kufanya jitihada binafsi za kuomba na hatimaye kufanikisha kupatikana kwa mafunzo hayo kwa watendaji wa ofisi yake pamoja na wanasheria wengine kutoka wizara na taasisi za serikali ambayo yameleta tija na faida kubwa kwa taifa na pia kukuza upeo na ufahamu wao katika namna bora ya usimamizi wa mikataba na kujifunza mbinu bora za kufanya mapatano.



**IRENE**

UKURASA 12

JUMAMOSI MEI 18, 2022

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



# MAMBO MANNE

## MAPACHA WANAOFANANA

KUNA vitu vingi vya kushangaza endapo utakutana na waigizaji wawili mapacha, Christina na Regina Mroni, ambao wamefanana.

Kupitia mahojiano yao kupitia EATV, wasanii hao wameeleza kwamba kufanana kwao kuna faida nyingi kuliko hasara na hivyo jambo hilo kwao linawanufaisha kimaisha.

Kwanza, mmoja wa wasanii hao anapopata kazi na kupata dharula hana hofu, kwa sababu pacha mwingine anakwenda kuifanya na kila mtu asigundue kuwa wanayemuona sio yule anayetakiwa.

"Sisi ni waigizaji pekee mmoja anaweza kufanya kazi ambayo alitakiwa kufanya mwingine na ikaenda vizuri bila kugundulika," amesema Regina.


Pili, wanapopita mtaani hakuna mtu anayetambua kuwa wapo wawili, hivyo inakuwa rahisi mmoja akasafiri au kwenda sehemu nyingine na watu wakaona wanaishi na mtu yuleyule.

Tatu, wanapohitaji kushona nguo, hawaitaji kwenda wote wawili, kwani mmoja anatosha kwenda na nguo zitakazoshonwa zikatumiwa na wote.

Jambo la nne ni kuwa wanaume wao kwa kawaida wanakuwa makini sana kwani wakifanya tofauti wanajikuta wamekosea. Kuanzia kukumbatia hata kubusu wanafanya kwa tahadhari kubwa wakihofia kuwachanganya.

BASI SAWA

## Irene Uwoya awasuta wapenda vya bure



MWIGIZAJI mkongwe wa Bongo Muvi, Irene Uwoya, amewashauri watu wasikimbilie makanisani kwenda kupata miujiza, wakati mioyo yao imejaa chuki na ubaya.

Kupitia video fupi aliyoiweka kwenye mtandao wa Instagram, Uwoya amesema kama ukiomba kwa haki na utaratibu ni rahisi kupata kwa sababu mbele ya Mungu hakuna dalali.

"Jifunze kuwa karibu na Mungu, jua kufunga, kusali na kutoa zaka unaona majibu mazuri. Kuna watu wana roho mbaya na wanakimbilia makanisani kupata miujiza huko ni kujiongopea ni lazima uwe karibu na Mungu ili upate unachotaka," amesema Uwoya.

## Shamsa hakika umesema



MSANII wa filamu za Bongo Muvi, Shamsa Ford, amesema hawezi kukata tamaa kwa sababu kila kitu anachokifanya anamtegemea Mungu.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Shamsa, ameandika kwamba Mungu anaweza kukupitisha njia yenye changamoto nyingi, lakini usipate tatizo lolote.

"Mungu wala hafananishwi na kitu chochote, anaaweza akakupitisha njia yenye mamba na wasikung'ate akiamua. Nakupa moyo unayepitia changamoto yoyote usikate Tamaa maana anakuona na anakusikia. Amini ipo siku kila kitu kitakaa sawa," ameandika.



## BABA LEVO KWA UTAFITI UPI?

MWANAMUZIKI na mtangazaji, Baba Levo, amesema wanawake wafupi wana tabia ya upendo, uvumilivu na wanadumu kawtika ndoa.

Akizungumza kupitia redio ya Wasafi, Baba Levo amewataka kila mwanaume mwenye mwanamke mfupi ni lazima amkumbatie kwa upendo kwa sababu wanajua kule familia.

"Kama mwanaume una mwanamke mfupi mkumbatie maana hao ndio wanajua kulea familia. Wanawake warefu weupe wao zao kucheza Amapiano na kupanda juu ya meza," amesema Baba Levo.



## Anjella hashikiki kwa singeli

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Anjella, amesema hatajutia uamuzi wake wa kugeukia Singeli, akisema huko ndiko anaona moyo wake unahitaji.

Akizungumzia hatua yake hiyo, Anjella amesema kwamba muziki wa Singeli ni unatoka ndani ya jamii za Uswahilini, mahali alipotoka na ndio maana ameamua kuukumbatia na kuachana na Bongo Fleva.

"Nimeamua rasmi kuingia kwenye muziki wa Singeli. Nina albamu tayari yenye ngoma 20 na zote ni Singeli. Singeli ni muziki wetu wa asili," ameandika Anjella kupitia ukurasa wake wa Instagram.

## BENDI 5 ZA MASHIRIKA YA UMMA

**Na Adam Fungamwango**

RAIS wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliweka sera na mifumo ambayo ilikuwa inajiongoza wenyewe, ikiwemo mambo ya utamaduni, sanaa na michezo kuanzia mashuleni, wizarani, kwenye taasisi mbalimbali, jeshini hadi kwenye mashirika ya umma.

Ndiyo maana wakati huo, mashirikia mengi ya umma yalikuwa na timu za mpira wa miguu, netiboli, mpira wa wavu, ngumi, bendi za muziki wa dansi na hata taarabu.

Ndicho kipindi ambacho Tanzania ilikuwa juu zaidi kwenye muziki, na mpira wa miguu.

Tunakuwa tunawaletea bendi mbalimbali za taasisi, viwanda, mashirika zilizovuma miaka hiyo kuanzia 1970, hadi mwishoni mwa miaka 1990.

Leo tutaanza na bendi ya Mashirika ya Umma, ambayo yaliunda bendi za muziki wa dansi na kutikisa anga ndani na nje ya nchi.

**STC Jazz Band**

Ni bendi iliyokuwa inamilikiwa na Shirika la Biashara ya Ndani, lililojulikana kama 'Stade Trade Corcoration', ikajulikana ka STC Jazz band.

Ndiyo bendi ya kwanza kupigia Marijani Rajab katika karia yake ya muziki, lakini pia Juma Ubao ndipo alipoanzia.

Ilivuma sana miaka ya 1970 na baadhi ya nyimbo za bendi hiyo ni, 'Mwanangu Shida', na 'Muleme Muleme', ulioimbwa kwa lugha ya kizaramo, utunzi wake mmoja wa waimbaji tegemeo wakati huo, Omari Mgogo.

**Biashara Jazz Band**

Ukweli ni kwamba pamoja kuwa ilionekana ni bendi nyingine, lakini ilirithiwa kutoka STC kutokana na mabadiliko ya shirika hilo.

STC, ilibadilishwa na kuwa Bodi ya Biashara ya Ndani, 'Board of Intenal Trade', vitu vyote vikarithiwa na BIT, ikiwemo bendi hiyo, na ikabadilishwa jina, ikaitwa Biashara Jazz Band.

Wakati huo Majirani alikuwa ameshaondoka kwenda kujiunga na Safari Trippers. Aliyebaki ni Ubao. Bendi hiyo ilitamba sana na vibao vyake kama 'Kipini cha Dhahabu','Posa Nitaleta', na nyingine nyingi.

**UDA Jazz band**

Shirika la Usafiri Dar es Salaam, ndilo lilikuwa linaimiliki bendi hii iliyokuwa maarufu na tishio na bendi nyingi hapa nchini.

Moja ya wanamuziki maarufu waliopitia bendi hiyo ni Mikidadi Seif, Seif Mtambo, Hamza Kalala, na Benovilla Antony.

Kibao vyao maarufu ni 'Tulele Tuboe,' ulioimbwa katika lugha ya kimwera, 'Nenda kaishi Salama', 'Nachunga Heshima' na nyinginezo.

**Bima Lee**

Ikitumia mtindo wa Magnet Tingisha, Bima Lee, kati ya bendi kubwa nchini Tanzania. Ilianzishwa katikati ya miaka ya 1970, na kutoa vibao kama 'Ombi', 'Clara', 'Peleleza', 'Sofi' na nyingine.

Mwaka 1984, ilichukua wanamuziki wakubwa kutoka DDC Mlimani Park na Vijana Jazz, kama Joseph Mulenga, Selemani Mwanyiro, Abdallah Gama, Shaaban Dede, Athumani Momba na Jerry Nashon 'Dudumizi', hapo ndipo ilipokwenda juu ya kilele cha mafanikio.

Nyimbo kama 'Baba Shani', 'Milionea wa Mapenzi', 'Pesa Zanisumbua', 'Makulata', zilitikisa anga la muziki na mashabiki wake. Bendi hii ilikuwa inamilikiwa Shirikika la Bima la Taifa NIC.

**DDC Mlimani Park Orchestra**

Hii ni moja ya bendi mbili kubwa zaidi na zenye mashabiki wengi nchini Tanzania, kama ilivyo Msondo Ngoma Music Band.

Ilianzishwa mwaka 1978, ikiwa asilimia 90 ya wanamuziki kutoka bendi ya Dar International.

Wamiliki wa awali walikuwa ni Chama cha Madereva Taxi Tanzania, TTTS, japo kuna watu wanakwenda mbali zaidi wakidai chama hicho kilikuwa kivuli tu, lakini iliundwa na Maafisa Usalama. Baadaye ilikabidhiwa kwa Shirika la Maendeleo la Dar es Salaam (DDC), ndipo ilipoanza kuitwa DDC Mlimani Park, badala ya Orchestra Mlimani Park. Ilianzishwa maeneo yanayofahamika kama Mlimani City kwa sasa, ndiyo maana lilipatikana jina hilo la Mlimani.

FILAMU

## Unyago:Mchawi mtu, paka katumwa

**Na Adam Fungamwango**

KWENYE baadhi ya jamii za Kiafrika huamini mnyama paka akilia usiku, basi ni dalili mbaya. Baadhi humuogopa wanyama hao, hasa wale wanaoonekana usiku.

Hata hivyo, kutokana na imani hizo, wengine wakaenda mbali na kuja na msemo kuwa hata kama paka ana ishara au dalili za uchawi.

Ukweli ni kwamba kama mnyama huyo ana ubaya wowote unaosemwa, basi atakuwa anatumwa tu na binadamu.

Binadamu anatumia njia ya kumpandikiza ubaya paka, yeye akijificha nyumba yake asinekane. Ndipo wakaja na msemo huu wa 'Mchawi binadamu, paka katumwa tu.'

Msemo huu unaakisi kile kilichomo kwenye filamu ya 'Unyago.' Ni filamu inayoonyesha kuwa wakati mwingine mtu anaweza kupata matatizo, mikosi na majanga kibao, lakini chanzo si mnyama yoyote anayetafsiriwa kuwa ana mikosa kama vile, paka au bundi, bali ni watu wa karibu wanaokuzunguka.

Filamu inaanza ikionyesha kuwa mama Batuli anataka binti yake Batuli achezwe unyago, lakini baba mtu anakataa. Anasema ni mila zilizopitwa na wakati.

Upande wa pili, kijana mmoja anaitwa Tuga anampenda Batuli. Lakini kuna msichana mwingine anaitwa Sikitu ambaye ni binti wa shangazi wa Batuli, naye anampenda Tuga.

Kinachotokea ni kwamba mama Tuga na mama Sikitu, wanafanya kila njia kuhakikisha Tuga anafunga ndoa na Sikitu na si Batuli.

Hata barua ya posa ilipopelekwa kwa kina Batuli, shangazi mtu hakumaliza hata hafla ya upokeaji barua hiyo, akaondoka upesi. Akaenda hadi kwa mama Tuga kumweleza kuwa mwanaye amekwenda kutoa barua ya uchumba kwa kina Batuli badala kuleta kwa binti yake Sikitu.

Wote wanakasirika na kwenda kwa mganga kwa lengo la kumdhuru Batuli.



Na kweli siku ya kutolewa, mwali anaanguka chini na kuzimia na sherehe zote zinavunjika. Anatibiwa anapona.

Lakini hiyo haimfanyi Tuga kuahirisha lengo lake la kumuoa Batuli. Anamuoa kwa lazima. Harusi imekwisha, mama mkwe hamtaki mke wa kijana yake. Chaguo lake lilikuwa ni Sikitu.

Tuga alikuwa bado anaishi kwa wazazi wake, akaanza ulevi ili kuondoa mawazo ya mama yake ambaye kila kukicha alikuwa akimtukana binti wa watu.

Ulevi ukasababisha awe anampiga mkewe. Mke akaona arudi kwao. Huku nyuma, rafiki zake wakamkalisha chini Tuga, wakimsihi aache ulevi na amrudie mkewe. Anafanya hivyo. Anaacha pombe, anarudiana na mkewe na kuamua kuondoka nyumba kwa mama yake, kwenda kuanza maisha mapya mbali na kijiji hicho akiwa na mkwe Batuli.

# Portable dawa ya deni kulipa

MWANAMUZIKI maarufu mwenye utata, Habeeb Okikiola, maarufu kama Portable, ametiwa mbaroni kwa madai ya kukataa kulipa deni kwa mfanyabiashara aliyemuuzia gari aina ya G-Wagon.

Jeshi la Polisi Jimbo la Lagos, lilitoa taarifa kwamba lilimkamata mwanamuziki huyo Jumanne, kulingana na mtandao wa ThePunch.

Inadaiwa wakati wa ununuzi wa gari hilo lenye thamani ya Naira milioni 27, Portable ililipa milioni 13 pekee na ilipotakiwa kulipa kiasi kilichobaki alikataa akidai gari ni bovu.

Hata hivyo, juhudi za kulipa deni hilo iliposhindikana, mfanyabiashara huyo huyo aliripoti suala hilo polisi.





## Evan alilia samaki wake

MWIGIZAJI maarufu kutoka Nollywood, Evan Okoro, aliangua kilio kutokana na serikali kubomoa bwawa lake la kufugia samaki.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, mwigizaji huyo alichapisha video inayoonyesha mabaki ya bwawa hilo katika shamba lake lililoko katika mji wa Asaba katika jimbo la Delta.

"Sio haki, nimeumia moyoni, kwa nini wanatufanyia hivi? Kila kitu kimekwenda shamba langu la samaki limetoweka, shamba langu limepotea," alilia.

## Skales hujapendwa wewe!

MSANII wa muziki kutoka Nigeria, Skales, amesema hawezi kusumbuka na mapenzi kwa kuwa hakuna upendo wa kweli duniani.

Akiongea kwenye kipindi kipya cha The Midday Show, aliulizwa kuhusu kukiri kwake hapo awali kuwa aliwahi kutoka kimapenzi na wanawake takriban 100.

"Mimi ni mwanaume aliyevunjwa moyo na siamini katika mapenzi tena, ninaamini tu kuwa wanadamu ni wabinafsi na hakuna upendo, kuna nia nyuma ya kila penzi kwa sasa," amesema.





## Undani watoto 13 wa Bob Marley

JE unatambua mwanamuziki maarufu wa Reggue kutoka Jamaica, Bob Marley na mkewe Rita wote walikuwa na watoto nje ya ndoa lakini wanawatambua kama wanafamilia wa mwanamuziki huyo?

Usichojua kuwa marehemu Bob Marley na mkewe walikuwa na watoto 13, lakini wote hawakuzaa pamoja ila kuna wengine wamezaliwa nje ya ndoa na kutokana na taratibu zao wanajulikana kama watoto wao wa kuwazaa.


Watoto hao ni Imani Marley, Sharon Marley, Cedella Marley, Ziggy Marley, Stephen Marley, Robert Marley, Rohan Marley, Karen Marley, Stephanie Marley,Julian Marley,Mani Marley, Damian Marley na Makeda Marley

## Wonder kawa raia Ghana

RAIS wa Ghana, Nana Akufo-Addo, amempa hadhi ya kuwa raia wa nchi hiyo mwanamuziki na mtunzi maarufu wa Marekani, Stevie Wonder.

Msanii huyo mkongwe na familia yake wamefanya ziara nchini Ghana na katika moja ya mapokezi aliyoyapata ni kukutana na kiongozi huyo na kwa heshima alimpatia uraia kamili.

Stevie Wonder aliwasiri nchini humo Jumatatu kama ndoto yake ya kukanyaga ardhi taifa hilo la Afrika ambalo anaamini ndiko kuna chimbuko lake.





## Yatima wapatiwa mahitaji muhimu

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

WATOTO yatima na waliokuwa wakiishi kwenye mazingira magumu kituo cha Light In Africa, katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, wamepatiwa msaada wa mahitaji mbalimbali ya kibinadamu.

Msaada wa mahitaji hayo,yalitolewa jana na Mwenyekiti wa Nyanza Group, Malimi Kija, alisema wametoa msaada huo, kwenye kituo hicho,kinacholelea watoto yatima na wanaoishi kwenye mazingira magumu.

Hata hivyo,alisema kikundi hicho, kimenunua vyakula, sabuni, mafuta na taulo za kike, kwa ajili ya watoto hao yatima na wenye kuishi katika mazingira magumu.

Mwenyekiti huyo alisema kikundi chao kina utaratibu wa kusaidia jamii kwa kile wanachokipata kupitia shughuli na kazi wanazozifanya kwa ajili ya vipato vyao.

"Fedha za kununua mahitaji yote haya wanachama wa Nyanza Group wamejitolea mifukoni mwao siyo kwenye mfuko wetu ni pale tulioguswa na kujitolea," alisema Kija.

Aidha, alisema pamoja na kutoa vyakula hivyo wana Nyanza Group pia wametoa fedha kwa ajili ya kununua maziwa ya kunywa asubuhi pamoja na chai.

Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani (TEO), Isack Mgaya, amewapongeza wadau hao wa maendeleo kwa kujitolea kusaidia watoto yatima na waliokuwa wanaishi kwenye mazingira magumu.

Alisema kitendo kilichofanywa na kundi hilo, kinapaswa kuigwa na wana vikundi wengine wa mji mdogo wa Mirerani katika kusaidia wahitaji.

"Misaada hii itumike ipasavyo kwa lengo lililokusudiwa na wana Nyanza Group ambao wamefanya jambo zuri la heri," amesema Mgaya.

Mmoja wa walezi wa Kituo cha Light In Africa, Mariam Mkali, aliwashukuru wana kikundi hicho,kwa kutoa msaada kwa watoto hao.

"Tunamshukuru Mungu kwa neema yake kwani watoto hawa wamekuwa marafiki kwetu na tunawasaidia kwa moyo mmoja, tunawapongeza nanyi kwa kuja kuwasalimia watoto hawa," alisema Mkali.

**Alisema kitendo kilichofanywa na kundi hilo, kinapaswa kuigwa na wana vikundi wengine wa mji mdogo wa Mirerani katika kusaidia wahitaji.**

# Uhamiaji yaonya mawakala wa wahamiaji haramu

**Na Oscar Assenga,** TANGA

JESHI la Uhamiaji limetoa onyo kwa mawakala wanaohusika kusafirisha wahamiaji haramu na kuwaingiza nchini.

Licha ya onyo hilo, jeshi hilo limesema watu hao siku zao zinahesabika, hivyo limetoa angalizo kwa wahusika kuacha mara moja kufanya biashara hiyo na kutafuta shughuli za kuwaingizia kipato halali.

Onyo hilo lilitolewa jana na Ofisa Uhamiaji Mkoa wa Tanga, Kagimbo Hosea, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na operesheni walioifanya kuanzia Mei 6 hadi 12, mwaka huu.

Alisema katika operesheni hiyo, walikuwa wakipambana na mawakala wa usafirishaji haramu wa binadamu ili kuhakikisha biashara hiyo inatokomezwa.

"Tulifanikiwa kupeana majukumu ya kuwasaka mawakala na tuna orodha ya mawakala 80 wanaojihuisha na biashara haramu ya usafirishaji na wengine bado wana kesi mahakamani huku wengine, uchunguzi ukiendelea, pia wako waliokwisha kuhukumiwa vifungo mbalimbali na tulifanikiwa kuwapata tunaendelea na mahojiano nao wakieleza wamekwisha kuachana na biashara hiyo," alisema

Ofisa huyo alisema kuwa Machi, mwaka jana, serikali iliondoa visa rejea kwa raia wa Ethiopia ili kuingia kwa utaratibu wa kawaida kwa kulipa visa mpakani na kuendelea na safari zao.

Hata hivyo, alisema waliamini suala hilo lingeondoa au kupunguza tatizo la wahamiaji haramu lakini bado inaonekana haikusaidia kutokana na idadi kuongezeka na takwimu walizonazo kwa muda wa miezi michache wahamiaji haramu 72 wamekatwa.

"Kati yao wako Waethiopia 57, Wasomalia sita Mkenya mmoja na Watanzania wanane, na Watanzania wanaofanya shughuli za kuwasafirisha wa wahamiaji haramu wameongezeka na tumekamata magari matatu, Toyota Land Cruse V8 lenye namba T.188 CAG, lori KAG 9665 lenye Trela ZDB 8244 na Toyota Noah T.264 DCC. Ukiangalia ongezeko bado linaendelea, hivyo tutaendelela kufanya opresheni kuhakikisha wanatokomeza mtandao huo," alisema

Alisema wakati wa operesheni hiyo, walikwenda maeneo ya Jasini, Ngomeni, Muheza Stendi, Duga, Maramba, Mkinga na maeneo mengine mkoa wa Tanga ikiwamo Daluni Kata ya Mbuyuni na walifanikiwa kuwakamata wahamiaji haramu watano ambao Wasomali ni watatu, Waethiopia wawili na Mtanzania mmoja ambaye alikuwa amewahifadhi kwenye nyumba yake wakisubiri kusafirishwa.

Aidha, alisema idadi kubwa wanaokamatwa ni raia wa Ethiopia na Wasomalia wakiwa wachache na baadhi ya Watanzania wanahusika kuwahifadhi na wengine wanapita kwenye maeneo yao lakini hawatoi taarifa.

"Shida kubwa ni madalali ambao wamekuwa wakiwaeleza kwamba Tanzania ni kugumu kuingia wakielekezwa na madalali kutoka nchini jirani jambo ambalo sio kweli kutokana na kwamba Serikali iliondoa visa rejea kwa raia wa Ethiopia ili kuingia kwa utaratibu wa kawaida kwa kulipa visa mpakani na kuendelea na safari zao," alisema Kagimbo.




Meneja wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira vijijini (RUWASA) mkoa wa Manyara, Mhandisi Walter Kirita (wa pili kushoto), akisoma taarifa ya utendaji kwa Mkuu wa mkoa huo, Queen Sendiga (katikati), wakati wa kikao kazi cha mamlaka hiyo, mjini Babati, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mtaalamu ataja sababu kuzaliwa na udumavu kondefu

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKURUGENZI Msaidizi wa Huduma za Lishe Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Luitfrid Nnally, amesema ulaji duni kwa wajawazito na kutokuzingatia makundi ya vyakula husababisha kuzaliwa kwa watoto wenye kimo kifupi, udumavu na ukondefu.

Nnally alisema hayo jana wakati akizungumza na wasindikaji wanaoongeza virutubisho kwenye unga wa mahindi mkoani Manyara.

"Watoto wenye kimo kifupi tatizo ni udumavu na ukondefu unasababisha mpaka mtoto kulazwa hospitalini. Ukondefu wakati mwingine unakuwa tofauti na umri wa mtoto,"alisema.

Aidha, alisema mkoa huo,umepunguza kiwango cha udumavu kutoka asilimia 36 mpaka asilimia 32 huku serikali ikiwa imepunguza udumavu mpaka asilimia 30 kitaifa.

Nnally alisema kwa Tanzania ukondefu uko kwa asilimia 3.3 na Shirika la Afya Duniani (WHO) linataka nchi iwe chini ya asilimia tano.

Mtaalamu huyo aliataja makundi ya vyakula ambayo wajamzito na mtu yeyote anastaili kutumia kuwa ni vyakula vya asili ya nafaka na mizizi mibichi ikiwamo mihogo na magimbi.

Alisema vyakula vingine vya asili ni wanyama mfano samaki, wadudu na Nyama, vyakula vya asili ya mikunde na mbegu mbalimbali mfano kunde na njegele, matunda ambayo ndio yanasaidia kutupatia vitamini.

Nnally alisema makundi mengine ni mboga ambazo zina madini joto ambayo yanaongeza damu, mafuta na maji safi na salama.

Awali, Mratibu wa Lishe, Grace Shileringo, kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia alisema chakula kinachotolewa shuleni hakina ubora ndio sababu serikali imekuja na mpango wa kurutubisha unga wa mahindi.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, aliagiza halmashauri mkoani humo, zihakikishe fedha za lishe zinatolewa na utoaji wa fedha za lishe sio hiari kuzitoa ni lazima.

Sendiga,alisema fedha za lishe,hazitakiwi kuchepushwa kwenda kufanya kazi nyingine kwa kuwa kuna maeneo mengine ambayo wakurugenzi hawajui fedha zinafanya nini.

Akitoa ufafanunuzi juu ya namna ya kuongeza virutubishi kwenye unga, Meneja mradi wa urutubishaji kutoka Shirika la Global Alliance for Improved Nation (GAIN), Archard Ngemela, alisema awali mashine za kuweka virutubisho zilikuwa zinauzwa hadi Shilingi Milioni tano.

"GAIN na SIDO wamesaidia upatikanaji wa mashine hadi Shilingi millioni 1.5 kwa sasa,"alieleza Ngemela.

Ngemela alisema halmashauri zinapaswa zinatenga fedha ya kununua mashine kupitia fedha za lishe.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Baraka Kanunga, alisema mashine za kuongeza virutubisho zipo tatu pekee japo mkoa mzima una mashine 14 tu.

Alisema angalau mashine zinatakiwa kuwepo tatu kila kata ili zisaidie kurahisisha upatikanaji wa huduma.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Enzi za kubandika picha ukutani vyumbani

## -Watoto wa mjini waliita 'geto'
## -Bruce Lee, Bob Marley, Pele, Michael Jackson walitikisa




**Na Adam Fungamwango**

NCHI hii imetoka mbali sana na watu wake nao wametoka mbali pia. Kwa sasa ukiingia kwenye chumba cha kijana wa kisasa, hata kama hutakuta vitu vingi, lakini unaweza kuona kuna feni, televisheni, redio, na shefu la kuwekea viatu.

Ukutani atakuwa amepiga rangi yoyote ile au chumba kimepigwa plasta ya 'gypsum.'

Kama vyote hakuna, basi utakutana na chumba kilichopigwa plasta ya simenti tu, na kama vile vyumba vya uswahilini kabisa, kule kwetu Manzese, Tandale, Mburahati, utakutana na matofali matupu.

Hii ni tofauti na zamani, miaka ya 1970, hadi katikati ya miaka ya 1990, ambapo vijana wa mjini wakati huo wakijiita 'mabitozi', wao hawakupaka rangi vyumba vyao, 'gypsum', wala nini na hata mtu akiingia atashindwa kujua ukuta wake ukoje.

Mabitozi wa wakati huo ambao kwa sasa wanajiita matozi,

**Kivutio kingine cha picha za rangi ambazo zilikuwa picha za mkali za muziki wa reggae, Bob Marley, ambaye kifo kilimkuta mwaka 1981.**

walikuwa wanabandika picha za kwenye magazeti, pamoja na majarida mbalimbali ambayo yalikuwa na picha za watu maarufu wakati huo.

Vijana wa sasa ambao wakishakuwa watanashati wanajiita matozi, hili jina hata baba na babu zao walilitumia miaka hiyo, wao walijiita mabitozi.

Kwa nini zamani walijiita mabitozi na sasa wamelifupisha na kujiita matozi? Na asili ya jina hili ni nini? Kwa nini vijana watanashati wa zamani walijiita mabitozi na wa sasa wanajiita matozi? Wiki ijayo tutawaeleza kila kitu. Leo tuendelee na mada yetu ya kubandika picha za magazeti na majarida ukutani.

Ikumbukwe kuwa picha hizo utazikuta kwenye vyumba vya vijana tu, na siyo mtu mzima ambaye tayari ana familia.

Walikuwa wanakata vipande vya magazeti vyenye picha halafu wanabandika ukutani kwa gundi ya maji au yoyote ile ambayo inaweza kufanya zikaganda kwenye ukuta wa vyumba vyao, wenyewe wakati huo waliyaita 'mageto.'

Hilo ni jina lililokuwa linatumika enzi hizo kwa vyumba vya vijana ambao wanaishi peke yao na hawajaoa. Na kama nilivyoandika ndiyo walikuwa na tabia ya kubandika picha mbalimbali ukutani.

Picha za magazeti ambazo zilikuwa kivutio kwao ni zile za wachezaji mbalimbali wa soka la Tanzania, kama vile Simba, Yanga, na zingine zilizokuwa maarufu kipindi hicho kama vile, Pamba FC, Nyota Nyekundu, Pilsner, Sigara, Tukuyu Stars, Waziri Mkuu, RTC Kigoma, RTC Kagera na zinginezo.

Pia picha zilizokuwa zinakatwa kwenye magazeti na kubandikwa zikiwa za wanamuziki mbalimbali za bendi kama Juwata Jazz Band, 'Msondo Ngoma', DDC Mlimani Park Orchestra,' Sikinde Ngoma ya Ukae', Dar International ya Marijani Rajab, Safari Trippers, Bima Lee, Urafiki Jazz, Kurugenzi Jazz, na nyingine nyingi.

Wakati huo pia kulikuwa na majarida mengi ambayo yenyewe yalikuwa ya rangi na yalionekana kuvutia zaidi yakibandikwa ukutani, tofauti na picha za magazeti ambazo zilikuwa na rangi nyeusi na nyeupe tu.

Majarida hayo yalikuwa ni ya watu maarufu hasa wa nje ya nchi. Nakumbuka wakati huo kulikuwa bado mashabiki wengi walikuwa wakipenda filamu za mbabe wa sanaa za mapigano, Bruce Lee, ayefariki mwaka 1973.

isingewezekana ukaingia kwa kijana yoyote ukakosa picha yake, hasa ile ambayo yupo kifua wazi, akiwa ameweka mikono yake tayari kwa mapigano, mashavu yake na mbavu zikiwa na mistari ya damu, inayotokana na kukwanguliwa na adui anayepigana naye.

Picha nyingine maarufu kwenye kuta za vyumba vya vijana wakati huo ni ya mfalme wa soka duniani, Edson Arantes do Nascimento, maarufu kama Pele, aliyevuma miaka ya 1970 na kufariki 2022.

Kivutio kingine cha picha za rangi ambazo zilikuwa picha za mkali za muziki wa reggae, Bob Marley, ambaye kifo kilimkuta mwaka 1981.

Mbali na watu hao maarufu, picha zingine ni za Michael Jackson, na wanamuziki wengine, wakiwemo wacheza mpira wa kikapu.

**Tuma meseji 0716 350534**



HABARI KIMATAIFA

# Afrika Kusini yazidi kuibana Israel

**NEW YORK,** MAREKANI

SERIKALI ya Israel imeishutumu Afrika Kusini kwa kuwasilisha "madai ya upendeleo na uongo katika mahakama ya Haki ya Umoja wa Mataifa.

Afrika Kusini ilifungua kesi katika mahakama hiyo ikitaka kusitishwa mashambulizi ya kijeshi katika mji wa Rafah kusini mwa Ukanda wa Gaza.

Mahakama ya Kimataifa ya Haki (ICJ) ilianza kusikiliza mashtaka hayo kwa siku mbili kuanzia Alhamisi, na Afrika Kusini iliiambia mahakama hiyo kwamba Israel inakusudia kuwafuta Wapalestina kutoka kwenye uso wa Dunia na kuiita Rafah kama msimamo wa mwisho.

Mawakili wa Israel waliwasilisha majibu yao mbele ya mahakama siku ya jana ikipinga mashtaka hayo na kuyaita ya uongo.

Tayari mahakama hiyo ilitoa uamuzi kesi iliyofunguliwa na nchi hiyo mwezi Januari, ikiishutumu Israel kwa kufanya mauaji ya halaiki dhidi ya Wapalestina katika Ukanda wa Gaza.

Katika mashtaka hayo, Afrika Kusini pia inataka kuilazimisha Israel kuruhusu upelekaji usio na vikwazo wa ndani ya Gaza kwa misaada, waandishi wa habari na wachunguzi.

Israel ilianza mashambulizi yake dhidi ya Hamas mjini Rafah siku 12 zilizopita, huku kukiwa na wasiwasi kutoka kwa Umoja wa Mataifa na mengine kuhusu hatari.

Zaidi ya watu milioni moja waliokimbia makazi yao walikuwa wamejihifadhi Rafah na zaidi ya 630,000 sasa wamekimbia mji huo tangu kuanza kwa operesheni hiyo, UN ilisema.

Wakati huo huo, Jeshi la Marekani limethibitisha kuwa shehena ya kwanza ya msaada imeingia katika ardhi ya Gaza kupitia gati ya muda iliyojengwa na nchi hiyo.

Kamandi Kuu ya Marekani ilithibitisha katika chapisho kwenye X kwamba malori ya misaada yalianza kusogea hadi kwenye bandari hiyo ya muda na kuanza kuchukua shehena hiyo na kupeleka kwa raia wanaohitaji.

"Hii ni juhudi inayoendelea, ya kimataifa ya kuwasilisha misaada ya ziada kwa raia wa Palestina Ukanda wa Gaza kupitia baharini," lilisema chapisho hilo.

Hata hivyo taarifa hiyo ilisema kwamba hakuna wanajeshi wa Marekani waliokwenda pwani ya Gaza.

Marekani ilianza kujenga kituo hicho wiki chache zilizopita ili kuwezesha kupeleka misaada Gaza, wakati Israel ikiendelea na kampeni yake ya kijeshi dhidi ya Hamas.

Tangazo hilo limekuja baada ya kuripotiwa Jumatano, mamia ya tani za msaada ziliwasili nchini Cyprus, na baadaye kupakiwa kwenye meli za kibiashara kwa ajili ya kupelekwa kwenye gati hilo.

Baada ya kufikishwa kwenye gati, meli ndogo za kijeshi za Marekani, zenye uwezo wa kubeba kati ya malori matano na 15 ya misaada, yataisafirisha hadi kwenye gati inayoelea, yenye urefu wa mita mia kadhaa, iliyowekwa kwenye ufuo wa Gaza.

Malori hayo yatasafiri kando ya gati hiyo kabla ya kushusha msaada kwenye yadi ya kupanga misaada iliyojengwa pwani.

Mamlaka zilisema kuwa Umoja wa Mataifa, kupitia Shirika la Mpango wa Chakula Duniani, litawajibika kwa usambazaji wa misaada hiyo.

**BBC**



Wanajeshi wa Ukraine wakikagua droni kabla ya kuirusha kwenda maeneo yanayokaliwa na Russia juzi. **PICHA: REUTERS**

# Russia, China ushirikiano mpya

**BEIJING,** CHINA

MARAIS Vladimir Putin wa Russia na Xi Jinping wa China wamekubaliana kuimarisha uhusiano wa nchi hizo na kuuita kama ushirikiano wa enzi mpya.

Rais Putin na Jinping waliahidi kuanza zama mpya ya ushirikiano katika kile kinachotafsiriwa kama kuungana dhidi ya mpinzani wao mkuu Marekani ambaye wanamuelezea kuwa mchochezi anayetaka kurejesha enzi za vita baridi na kusababisha machafuko duniani kote.

Kiongozi huyo wa Russia yuko katika ziara ya siku tatu nchini China, alipokewa kwa heshima za kiitifaki na kijeshi.

Rais Jinping Xi aalimwambia Putin kuwa uhusiano kati ya nchi hizo mbili umepatikana kwa tabu na kwamba pande zote zinapaswa kuutunza na kuuenzi.

Viongozi hao wawili wametia saini taarifa ya pamoja ambayo inadhihirisha wazi upinzani wao kwa Marekani kuhusu mambo mbalimbali ya kiusalama na kimkakati, Taaruifa hiyo iligusia mvutano kati ya China na kisiwa cha Taiwan, vita vya Russia nchini Ukraine, misimamo kuhusu Korea Kaskazini, mahusiano ya kibiashara na ushirikiano wa teknolojia mpya ya nyuklia.

Itakumbukwa kuwa mnamo Februari 2022, China na Russia zilitangaza azma yao ya kuwa na ushirikiano usio na kikomo, wakati Putin alipotembelea nchi hiyo siku chache kabla ya kuivamia Ukraine.

Rais Putin alimshukuru Jinping kwa juhudi za kutatua mzozo unaoendelea nchini Ukraine.

Hata hivyo, Jinping aliema nchi yake inataraji kuona bara la Ulaya likirejea hivi karibuni katika hali ya amani na utulivu na kuongeza kwamba China itatekeleza jukumu muhimu la kufanikisha hilo.

Alisema nchi yake iko tayari kushirikiana na Russia ili kufikia maendeleo na ustawi wa pande zote na kwa pamoja wamejitolea kusimamia uadilifu na haki ulimwenguni kote.

## Raia watakiwa kulinda mji uliozingirwa Sudan

**DARFUR,** SUDAN

GAVANA wa jimbo la Darfur magharibi mwa Sudan, Minni Minnawi, amewataka raia kuchukua silaha ili kuulinda mji mkuu wa eneo hilo, El-Fasher, kutoka kwa waasi wa Rapid Support Forces (RSF), ambao wameuzingira kwa wiki kadhaa.

Zaidi ya watu 60 walifariki na mamia kujeruhiwa tangu mapigano yalipoanza Mei 10, kulingana na shirika la misaada la kimatibabu la Madaktari Wasio na Mipaka.

"Tunatangaza kuwepo kwa tahadhari ya jumla ya kutetea maisha na mali ya raia wasio na hatia huko El Fasher," Bw Minnawi alisema katika chapisho kwenye mtandao wa X .

Kiongozi huyo alikuwa akijibu wito kama huo uliotolewa na RSF, iliyosema imezindua kampeni mpya ya kuhamasisha wapiganaji kutoka mikoa yote kuvamia mji huo.

Hata hivyo, RSF,ilikataa madai hayo na badala yake ikamshutumu gavana huyo kwa kuchochea mifarakano ndani ya Darfur.

Vikosi vya kijeshi na jeshi la Sudan, likisaidiwa na makundi yenye silaha ya Darfur, wameendelea kulaumiwa kutokana na kuongezeka kwa mapigano El Fasher.

Mratibu wa masuala ya kibinadamu wa Umoja wa Mataifa nchini Sudan, Clementine Nkweta-Salami, ameonya kwamba kuendelea kwa ghasia kunatishia maisha ya watu zaidi ya raia 800,000.

Vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini humo vilianza mwezi Aprili mwaka jana na juhudi za kimataifa za kusuluhisha mapigano kati ya vikosi hasimu zimeshindikana. **BBC**

# Bandari Kwala kuhudumia makontena 300,000

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Bandari Tanzania (TPA), imesema Bandari Kavu ya Kwala iliyoko Mkoa wa Pwani inatarajiwa kuwa na uwezo wa kuhudumia shehena ya makasha 300,395 kwa mwaka yanayokwenda nchi jirani.

Hayo yamo kwenye taarifa ya Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Plasduce Mbossa, iliyokuwa ikielezea maendeleo ya ujenzi wa bandari hiyo ambayo imeshaanza kupokea makasha matupu na yenye shehena.

Taarifa ilisema kwa mwaka bandari hiyo kavu itakuwa na uwezo wa kuhudumia makasha 823 kwa siku na makasha 300,395 kwa mwaka sawa na asilimia 30 ya makasha yote yanayohudumiwa na bandari ya Dar es Salaam kwa sasa.

Katika kuhakikisha Bandari Kavu ya Kwala inakuwa tayari kutoa huduma kwa shehena mbalimbali, taarifa ilisema TPA imepata leseni ya bandari kavu inayotolewa na Mdhibiti wa Usafiri Majini, Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania na Leseni ya Forodha inayotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).




Ilisema kwa sasa takwimu mpaka Februari 10, mwaka huu, kuna makasha 232 yenye mzigo na makasha matupu 78 yaliyokuwa yamekaa katika bandari ya Dar es Salaam kwa muda wa zaidi ya siku 50 yalihamishiwa katika bandari kavu ya Kwala na zaidi ya makasha 100 yamechukuliwa na wateja.

Puia taarifa hiyo ilisema taratibu za kuhamisha mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salaam kwenda Kwala zinaendelea kama sehemu ya kupunguza msongamano.

Ilitaja manufaa ya kuanza kwa shughuli za bandari kavu hiyo kuwa ni pamoja na kuongeza ufanisi na kiasi cha shehena inayohudumiwa katika bandari ya Dar es Salaam na kuongezeka kwa mapato ya Serikali kupitia huduma zitolewazo katika bandari za Dar na Kwala.

Alisema itapunguza gharama za uendeshaji hivyo kuvutia wateja kutumia bandari ya Dar es Salaam, kuongeza ushindani wa bandari ya Dar es Salaam kikanda kwa kuzingatia uwekezaji wa bandari za nchi jirani katika bandari kavu.

Alisema itasiaidia kuimarika kwa shughuli za kiuchumi na biashara za mikoa ya Dar es

Salaam na Pwani kwa kupunguza msongamano wa magari uliopo sasa na kuimarishwa kwa usalama barabarani kwa kuwa idadi kubwa ya shehena ya bandari ya Dar es

Salaam kutumia usafiri wa reli.

Ilisema itasaidia kuwa na maisha marefu ya miundombinu ya barabara za mikoa ya Dar es Salaam na Pwani na itaongeza ajira kwa wakazi wanaoizunguka Bandari Kavu ya Kwala na Taifa.

Ilisema kutakuwa na ongezeko la viwanda katika eneo la Kwala vitakavyovutiwa na uwepo wa bandari kavu na usafiri wa uhakika kuelekea lango kuu la biashara nchini bandari ya Dar es Salaam.

# Wapendekeza wagombea uongozi kutoenguliwa

**Na Restuta James**

KAMATI ya dini mbalimbali (ISCEJIC) imependekeza maboresho mawili makubwa kwenye sheria mpya za uchaguzi pamoja na ya Tume Huru ya Uchaguzi (INEC) ili makosa madogo yasiwaengue wagombea katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu na uchaguzi mkuu mwakani.

Aidha, imependekeza mabadiliko yatakayoibana INEC kisiwapo kisingizio chochote cha kuzuia mawakala wa vyama kuingia kwenye vituo vya kupigia kura jambo litakaloondoa dosari zinazosababisha malalamiko na uvunjifu wa amani wakati na baada ya uchaguzi.

Wakili Uzima Justin, ambaye pia ni mtaalamu wa katiba, aliyasema hayo jana Dar es Salaam alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari wakati wa mjadala wa mabadiliko ya sheria za uchaguzi ulioangazia utafiti kutoka nchi zingine za Afrika.

Alisema uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka 2019 na uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, ulikithiri kwa wagombea kuenguliwa kwa makosa madogo madogo na mawakala kuzuiwa kuingia vituoni, jambo lililoibua malalamiko.

Alitoa mfano wa Kenya na Afrika Kusini kwamba makosa ya mgombea kukosea kujaza tarehe ya kuzaliwa si kigezo cha kumwondoa kwenye kinyang'anyiro badala yake tume humwelekeza na kusahihisha kabla hazijaanza kupitiwa rasmi.

Alisema nchini Kenya, mgombea anaweza kujaza fomu kwa mtandao ambayo inampa ripoti ya makosa aliyofanya na kwa wale wanaojaza na kuziwasilisha kwenye ofisi za tume kwa mkono, mtumishi huzikagua na kuhakikisha hazina makosa madogo.

"Tunaona kwamba tume iweke utaratibu wa kuwasaidia wagombea kuhakiki na kusahihisha makosa madogo kabla ya mchakato. Tukifanya hivi, malalamiko ya kuengua wagombea kwa kosa la kiutawala yataisha," alisema.

"Kwenye uchaguzi za mwaka 2019 na 2020 tuliona jinsi wagombea walivyopata shida kurejesha fomu wengine wanakuta ofisi zimefungwa, wengine wanaambiwa muda umeisha... haya yanaweza kutatuliwa kwa sheria kuibana tume kutimiza wajibu wake kikamilifu," aliongeza.

Kuhusu vituo vya kupigia kura, alisema: "Tukirejea uchaguzi wa 2019 na 2020, tunakumbuka jinsi ambavyo mawakala wa vyama walivyozuiwa kuingia, walinyimwa fomu za matokeo na kwenye maoeneo mengine walishindwa kushuhudia zoezi la kuhesabu kura, ndio maana tunaona walau kwa sasa maeneo haya mawili ni muhimu yakarekebishwa na kuingizwa kwenye sheria kabla hatujaingia kwenye uchaguzi mwaka huu na mwakani."

Alisema mabadiliko yalitambua NEC kuwa huru hayajakidhi kiu na matakwa ya wananchi wengi kwa kuwa muundo wake hauko huru.

Alitoa mfano wa tume ya Afrika Kusini kwamba mwenyekiti wa kamati ya usaili wa wajumbe wa tume ni Jaji Mkuu ambaye anapatikana kwa kuomba nafasi hiyo na kupita kwenye usaili.

Alisema kadhalika wajumbe wengine wa kamati hiyo ni wakuu wa taasisi ambao wanapatikana kwa kuomba na kuhojiwa na chombo huru.

"Hapa kwetu tunajua majaji wote mpaka Jaji Mkuu wanateuliwa, Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu ambaye kwenye hii sheria ni mjumbe naye ni mteule wa Rais, unaona kwamba tumenakili muundo wa tume ya Afrika Kusini lakini siyo mfumo ulioiunda," alisema Uzima.

Kwa mujibu wa Uzima, nchi nyingine za Afrika zenye tume huru ni Ghana, Namibia na Mauritius.

Mshauri wa masuala ya sheria wa ISCEJIC, Wakili Gloria Mafole, alisema pamoja na kwamba inaitwa tume huru ya uchaguzi, haiko huru kimuundo, kibajeti na kiutendaji.

Alisema bado sheria zimempa rais mamlaka makubwa ya muundo wa tume na pia haijatoa uhuru wa kupinga matokeo ya urais mahakamani wala kwenda kwenye vyombo vya kisheria pale mgombea anaponyimwa haki ndani ya tume.

Naye Padre Chrisantus Ndaga, alisema uchaguzi ni nguzo muhimu ya kuwaleta wananchi pamoja na kwamba pamoja na changamoto zilizopo, tume itakuwa huru kwa kuwa serikali imekubali kuboresha sheria hizo.

huo ulikuwa ukichambua Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Sheria ya Tume ya Uchaguzi na ile ya Vyama vya Siasa, ambazo zilipitishwa mapema mwaka huu.

# Kamati Bunge yalia riba kubwa mikopo

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

KAMATI ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii imeshauri serikali kupunguza riba kwenye mikopo ya wafanyabishara wadogo kwa kuwa itasababisha wengi kushindwa kukopa kutokana na hali zao kiuchumi.

Katika mwaka 2023/24, serikali imesema itaipatia benki ya NMB Sh. Bilioni 18.5 kwa ajili ya kutoa mikopo yenye riba nafuu ya asilimia saba.

Akiwasilisha maoni ya kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwenyekiti wa Kamati, Fatma Toufiq, alisema kutokutolewa kwa fedha kwa ajili ya mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyabiashara hao kwa miaka miwili mfululizo kunaathiri juhudi za serikali za kuwawezesha kundi hilo kujikwamua kiuchumi.

"Aidha, kamati inaona kuwa kiasi cha riba cha asilimia saba ya mikopo kinachopendekezwa na wizara ni kikubwa ukilinganisha na hali ya uchumi wa wafanyabiashara wagodo wadogo hali itakayosababisha wafanyabiashara wengi kushindwa kukopa," alisema.

Alishauri serikali kutoa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya mikopo nafuu kwa wafanyabiashara ndogo kabla ya Mwaka wa Fedha kuisha ili kuwawezesha kukuza mitaji yao na kufanya mapitio ya kiasi cha riba ya mikopo hiyo ili wafanyabiashara wengi zaidi wakope.

"Kupunguza kwa fedha za uratibu wa wafanyabiashara hawa kutoka Sh. Bilioni 18.5 hadi Sh. Bilioni 10.5 kwa mwaka 2024/25, hakuendani na uhalisia uliopo wa uhitaji wa mikopo kwa Wafanyabiashara hawa," alisema.

Alishauri serikali iongeze bajeti ili kuwanufaisha wafanyabiashara wengi zaidi na iandae mkakati wa kutoa elimu juu ya faida za kujisajili na manufaa yatokanayo na usajili huo.

Oo

## HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa na maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri.
Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging.
Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani.
Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-13

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Alifika mapema mno. Saa nzima kabla ya Teddy kufika. Lengo ni lile lile. Pamoja na kumuamini Teddy, lakini kanuni moja ya ushushushu inasema usimumini mtu yoyote, hata kama ni baba au mama yako mzazi. Hiyo tu ilitosha kumuelekeza kuwa hata Teddy asiaminike. Hata kama si yeye kutumwa, lakini anaweza kuwa kuna watu wanafutilia nyuma, hasa baada ya kutoka nyumbani kwake kuchukua vitu vyake na kumletea pale alipo.

"Umeshafika?" Kamal alimuuliza kwa njia ya kumpigia simu. "Bado ila niko njiani karibuni nifike, wewe je?" "Mimi ndiyo bado kabisa." "Basi mimi nitakusubiri." "Sasa unasikia Teddy, ukifika kaa pale kwenye benchi la kituo cha mwendokasi hapo, mimi nitakukuta hapo hapo." "Sawa shemeji." Akaitikia Teddy.

Wakati Teddy anafika maeneo hayo na kuingia moja kwa moja hadi kwenye mabenchi ya kituo cha mabasi ya mwendokasi, Kamal alikuwa tayari ameshafika dakika 20 kabla.

"Ndiyo nafika saa hizi." Teddy alimjulisha kwa njia ya simu. Alichoshindwa kutambua ni kwamba tayari Kamal alikuwa ameshamuona. Hakumjibu kwa simu, kwa sababu alijua sauti za magari na vitu vingine vitakavyokuwa nyuma ya sauti yake vinaweza kumjulisha kuwa yupo maeneo jirani.

Alimjibu kwa meseji. "Mimi bado nipo njiani, ukae hapo hapo nilipokwambia, nitakukuta."


Alichofanya ni kuangalia kama Teddy alikuwa ameongozana na watu wengine, au kuna wanaomfuatilia nyuma.

Kwa jinsi alivyojifunza mwenyewe kwa kuangalia filamu za kipelelezi na kusoma vitabu, alijidhihirisha kuwa Teddy hajaongozana na mtu yoyote hata kama wameachana pale, na pia hakuna mtu anayemfutilia nyendo zake.

Alikuwa amesimama kando ya barabara ya Morogoro, upande ambao unatokea maeneo ya Magomeni Kota. Hakuvuka barabara. Alisubiri mpaka dakika 15 hivi, akamwambia akampigia simu atoke ndani ya jengo la mabasi ya mwendokasi.

"Mimi niko huku ng'ambo, nakuomba utoke humo ndani, si unajua macho ya watu tena, wasione unavyonipa hivyo vitu." "Sawa shemeji nakuja." Akajibu.

Lengo lake ni lile lile, kuona kama Teddy anafuatiwa na watu. Kitendo cha kutoka na kuvuka barabara kinaweza kwa mara nyingine tena kujidhihirishia usalama wake. Kwa upande wa Teddy yeye aliona ni sawa alichokifanya shemeji




**"Nipo hapa katikati ya vibanda vya mawakala wa simu na kioski." Akaongea kwa utulivu. Huku akimtazama kwa makini shemeji yake aliyokuwa amemaliza kuvuka barabara na kutembea kwa maringo mithili ya twiga mbugani.**

yake, kwa sababu isingependeza macho ya watu kuona nyaraka anazompa.

"Nipo hapa katikati ya vibanda vya mawakala wa simu na kioski." Akaongea kwa utulivu. Huku akimtazama kwa makini shemeji yake aliyokuwa amemaliza kuvuka barabara na kutembea kwa maringo mithili ya twiga mbugani.

Picha ilimrudisha nyuma na kuanza kumkumbuka mkewe Mariamu. Pamoja na kwamba hawakuzaliwa tumbo moja, Mariamu alizaliwa na mkubwa, na Teddy mdogo, lakini walifanana sana. "Yaani kama mapacha." Akaongeza mwenyewe bila kujijua. Alichoona ni kama mzimu wa mkewe ukija kumtembelea. Akili ikamkumbusha kuwa haukuwa wakati wa kumkumbuka mkewe au kumuwaza, bali ni kujilinda na wanaomsaka kwa tuhuma za kumuua mkewe. Kwa maana hiyo ni lazima awe makini "Nipo hapa shemeji." Akamwita. Teddy akamuona shemeji yake. "Shikamoo." "Marahaba." Wakati huo wote, Kamal alikuwa anamuagalia shemeji yake, wakati huo huo, kuangalia kama kuna mtu ambaye anaonekana kuvutiwa na wao kusimama pale.

Hakuona hilo. Nyuso chache zilizoonekana kuangalia, zikikuwa zinashangaa au kuvutiwa na uzuri ya Teddy.

Kamal alimshika mkono Teddy, halafu akamwambia. "Umepata vyote ambavyo nimekwambia uniletee?" "Ndiyo kwa bahati nzuri kila kitu kimekipata."

Mkononi alikuwa na bahasha kubwa, ambayo alimkabidhi. "Samahani shemeji yangu, najua kila tulipokuwa tunakutana, tukiwa pamoja hata na dada yako, tunakwenda sehemu tunakula, tunakunywa, lakini leo haitowezekana kutokana na mzingira. Angalia leo tumesimama juani, kama wasafiri ambao basi lao limeharibika wanasubiri litengenezwe."

"Najua shemeji, ila..." Akaanza kuangua kilio, lakini cha kimya kimya ambacho hakikuweza kuvutwa watu. "Ila nini shemeji?" "Mimi nachukia ndugu zangu na familia yote inavyokusema vibaya kuwa umemuua dada kwa ajili ya wivu, mimi kila nikitetea wapi, nazidiwa nguvu. Sasa niambie ukweli leo, shemeji kweli umemuua dada? Najua unatafutwa na Jeshi la Polisi, na picha zako zimeanza kutolewa kwenye magazeti, na dau nono limetangazwa..."

"Najua najua, usilie shemeji yangu. Hivi wewe unaamini kweli kwamba naweza kumuua dada yako?" Teddy akakataa kwa kutumia kichwa. "Basi amini kuwa mimi sijamuua dada yako, na nisingeweza kufanya hivyo kwa sababu yoyote. Wewe mwenyewe unajua jinsi tulivyokuwa tunapendana." "Sasa kwa nini usingiziwa?" "Teddy, najua kuna mtu au watu nyuma ya hili, na wameingia hadi ndani ya Jeshi la Polisi kuwarubuni wale wachache ambao wana tamaa ya pesa, wala rushwa kwa ajili ya kunisingizia, ili wao wawe salama." Akajibu huku akimfuta machozi Teddy kwa leso yake laini. "Sasa nini kitasababisha ulimwengu wote unaoamini wewe ni muuaji, kuwa hujafanya hivyo? Kama Jeshi la Polisi limeshasema wewe muuaji, nani sasa atapinga?" Akauliza Teddy kwa huzuni, na alionekana kumuonea huruma shemeji yake.

"Naamini ipo siku ukweli utabainika na waliofanya hivyo watafahamika hata kama baada ya miaka 100 kupita. Wao na mimi tunaweza kuwa hatupo tena duniani, lakini ulimwengu ukajua nini kilitendeka." Maneno haya yalimfanya Teddy kutaka kulia kwa sauti, lakini Kamal akamkataza na kumwambia kitendo hicho kitasababisha kujaza watu na wakamfahamu, licha ya kofia kubwa na mawani waliyovaa kuficha sehemu kubwa ya sura yake. Teddy akanyamaza, lakini ni kama alikuwa anaishiwa nguvu. Kamal alimshika mkono na kwenda kukaa kwenye viti vya kioski na kuagiza maziwa ya moto.

"Sasa wewe unaenda wapi na utajificha mpaka lini shemeji?" Teddy akauliza swali zuri na muhimu, lakini lilikuwa gumu.

"Mpaka sasa sina pa kwenda. Ninachofanya ni kuwakwepa tu askari, nikisubiri siku ambayo ukweli utafahamika." "Lini sasa?" Akauliza kwa nguvu na msisitizo.

Kamal, akamwambia. "Teddy, wala siyo muda mrefu, kila kitu kitajulikana. Nikwambie tu humo humo ndani ya Jeshi la Polisi, wapo askari wengi wema sana, wamesema watanisaidia ili ukweli ufahamike." Akamdanganya. Kidogo Teddy akaonekana kutulia. "Haiwezekani Damu ya Mariamu, iende hivi hivi, nakuapia, wote waliohusika watabainika. Hapo ndipo nitakuwa nimemzika Mariamu wangu, naye atakuwa amepumzika kwa amani, baada ya hapo baadaye nitatafuta mke mwingine wa kuoa. Na mke huyo ni lazima awe na vigezo kama alivyokuwa navyo Mariamu." "He! nani tena huyo?" "Ni wewe. Sitotaka kwenda kwingine, nitakuoa Teddy wewe ili kumuenzi Mariamu." "Teddy hakuamini kama maneno hayo yanatoka kwa Kamal. Alionekana kufurahi kana kwamba itafungwa mwezi ujao.

"Nitakuombea kwa Mungu jambo hili lifanikiwe ili utimize ulichoniahidi." Akasema akianza kulia tena. Safari hii machozi ya furaha.

**Itaendelea Jumamosi**

HABARI MICHEZO

# AZAM : YANGA KUTOPATA MGAO FEI TOTO AKIUZWA

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Azam FC uko tayari kumuuza kiungo mshambuliaji wake, Feisal Salum ‚Fei Toto' kwa sababu inaamini soka ni ajira na biashara.

Hata hivyo Azam FC imeweka wazi endapo watamuuza nyota huyo kwa klabu yoyote ya ndani au nje ya Tanzania, waajiri wake wa zamani, Yanga hawatapata mgao wowote.

Azam imetoa kauli hiyo baada ya kuwapo na tetesi Fei Toto akiuzwa, Yanga itajipatia mgao wa Dola za Marekani milioni 1.5 wakati thamani ya nyota huyo ni Dola za Marekani milioni mbili.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Azam FC, Hashim Ibwe, alisema watafurahi kuona kiungo huyo anauzwa kwa sababu atakuwa anaendelea ‚kupiga hatua' katika kazi yake.

Ibwe alisema walipomsajili Fei Toto kutoka Yanga hakuna makubaliano yoyote waliyowekeana na klabu hiyo baada ya kumnasa Mzanzibari huyo.

"Sio kweli kama Fei Toto atakapouzwa, Yanga watapata kiasi cha fedha cha Dola za Marekani milioni 1.5, hakuna makubaliano hayo, tulipoandikishiana zaidi ya kutoa fedha na kumpata kiungo huyo.

Kama kuna klabu inauwezo wa kununua mkataba wa nyota huyo iwe hapa Tanzania, Morocco, Afrika Kusini au mataifa mingine, milango ipo wazi waje, tufanye biashara," alisema Ibwe.

Aliongeza kikosi cha timu hiyo tayari kimefika Mwanza na wanaendelea na maandalizi ya mchezo wa nusu fainali ya Kombe la Shirikisho la CRBD Bank dhidi ya Coastal Union. Azam FC wanakuwa nyumbani kuwakaribisha Coasta Union kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza wakati kesho mabingwa watetezi watavaana na Ihefu kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid ulioko Arusha.



Mkuu wa Tigopesa, Angelica Pesha (kushoto), akionyesha promosheni mpya ya huduma ya Tigopesa katika simu. Kulia ni Mwandishi wa Habari, Milard Ayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mzungu Yanga Princess afunguka

**Na Saada Akida**

KIUNGO mshambuliaji wa Yanga Princess, Kaeda Wilson, amesema anafurahi kuwa sehemu ya kikosi cha timu hiyo na ameahidi ataendelea kupambana ili kuhakikisha wanavuna pointi 12 katika michezo minne ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyobakia.

Yanga inashika nafasi ya nne katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama 24, imebakiza mechi mbili za ugenini dhidi ya Bunda Queens na Geita Gold Queens, huku nyumbani watawaalika Alliance Girls na Baobab Queens.

Kaeda aliliambia Nipashhe ligi imekua na ushindani mkubwa kwa sababu kila timu imekuwa vizuri lakini wanaendelea kupambana kusaka matokeo mazuri katika kila mchezo uliopo mbele yao.

Aliongeza anaimani na ushirikiano mzuri wa wachezaji wenzake itasaidia kufikia malengo hayo ikiwamo kushinda mechi ambazo zipo mbele yao.

"Nafurahi kuwa Yanga, ushirikiano wa wachezaji wenzangu utatusaidia kufanya vizuri katika mechi zilizosalia. Mwanzoni hatukufanya vizuri na kushindwa kumaliza katika nafasi mbili za juu, lakini tunanafasi ya kumaliza kwenye nne bora," alisema kiungo huyo.

Aliongeza anapenda sana kuona anasaidia timu yake kupata matokeo mazuri kwa kucheza katika kiwango cha juu, kufunga mabao au kutoa pasi ya mwisho.

Kiungo huyo alisema anajifunza mbinu za uchezaji kwa kumfuatilia kiungo mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki, na kupelekea kuwa msaada kwa timu yake.

# Tanzania yajipanga kulibakisha taji u-15

**Na Somoe Ng'itu**

KOCHA Msaidizi wa Timu ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 15, Hilda Masanche, amesema kikosi chao kiko tayari kupeperusha vyema bendera ya Tanzania katika mashindano ya kimataifa ya CAF African Schools Football Championship, imeelezwa.

Mashindano hayo yanatarajia kufanyika kuanzia Mei 21 hadi 24, mwaka huu huko Zanzibar.

Masanche, nyota wa zamani wa Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Star) aliliambia gazeti hili kila mchezaji yuko tayari na imara kwa ajili ya kupambana na hatimaye kufanya vizuri kwenye mashindano hayo.

„Wachezaji wako vizuri na wanatamani mashindano yaanze hata leo (jana), wanasema wanatarajia kutupa matokeo chanya na kuendeleza matunda yaliyoonyeshwa na wawakilishi wa Tanzania mwaka jana huko Afrika Kusini," alisema kocha huyo.

Mashindano hayo yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), yatashirikisha timu za wasichana na wavulana 12, mbili kutoka katika kila upande.

## Maendeleo yajiweka pabaya Ligi Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BAADA ya kuruhusu kupokea kichapo cha mabao 7-2 kutoka kwa KVZ, Timu ya Maendeleo FC imejiweka katika hatari ya kushuka daraja kutokana na kushindwa kupata matokeo chanya kwenye Ligi Kuu Zanzibar inayoelekea ukingoni.

Maendeleo kutoka Pemba ilipanda daraja msimu uliopita na huenda ikawa ni timu iliyocheza ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Zanzibar katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa msimu mmoja tu.

Katika michezo 24, Maendeleo ambao wanaburuza mkia, wameshinda michezo minne, ikitoka sare michezo mitatu na imefungwa michezo 17, kibindoni ina pointi 15. Endapo Maendeleo watashinda michezo yao sita iliyobakia watafikisha pointi 33, jambo ambalo halipewi matumaini na hata viongozi wa timu hiyo.

Wakati huo huo Bodi ya Ligi Kuu Zanzibar imetangaza mechi za Ligi Kuu Visiwani humo zimerejea kwenye uwanja wa New Amaan Complex kuanzia mzunguko wa 24 baada ya uwanja huo kufunguliwa tena kuanzia juzi.

## ZISIKUPITE

### CASEMIRO ANUKIA SAUDIA

KLABU za Ligi Kuu ya Saudia (Saudi Pro) zimeonyesha nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Manchester United na Brazil, Casemiro mwenye umri wa miaka 32 na kiungo wa kati wa Ureno mwenye umri wa miaka 29, Bruno Fernandes. ***(Telegraph)***

### WALTERS KUONDOKA ARSENAL

ARSENAL inakaribia kumpoteza mlinzi, Reuell Walters, mwenye umri wa miaka 19, baada ya mchezaji huyo wa kimataifa wa England kukataa ofa ya mkataba mpya ili kutafuta nafasi ya kucheza kwingineko. ***(Athletic)***

### TRENT ATAJWA MADRID

REAL Madrid bado wameonysha nia ya kumsajili mchezaji wa kimataifa wa England, Trent Alexander-Arnold, mwenye umri wa miaka 25 kutoka Liverpool. ***(Fabrizio Romano kupitia Football365)***

### ALONSO KIBARUANI ULAYA

KOCHA wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso, anatumaini kusimamia klabu zake zote tatu za zamani za Liverpool, Real Madrid na Bayern Munich lakini hana uhakika ni kwa utaratibu gani. ***(Abendzeitung)***

### PALACE YAIBANIA BAYERN

NIA ya Bayern Munich kumnunua kocha wa Crystal Palace, Oliver Glasner, ilififia baada ya klabu hiyo ya Bundesliga kuambiwa itawagharimu pauni milioni 86. ***(Bild)***

### CONTE ANUKIA NAPOLI

NAPOLI imeanzisha tena mazungumzo na Antonio Conte kuhusu kuwa kocha wao baada ya kupunguza mahitaji yake ya mshahara, huku AC Milan pia ikitaka kuzungumza na Mtaliano huyo aliyewahi kufundisha Chelsea na Tottenham. ***(Il Mattino)***

### RAMOS KUTUA MAREKANI

MLINZI wa zamani wa Sevilla na Timu ya Taifa ya Hispania, Sergio Ramos, mwenye umri wa miaka 38, amepiga hatua katika mazungumzo yake klabu ya San Diego FC kuhusu kuhamia Ligi Kuu ya Soka ya Marekani. (MLS). ***(Athletic)***

### COLE SOKONI ENGLAND

BEKI wa zamani wa Timu ya Taifa ya England na klabu za Ligi Kuu England, Arsenal na Chelsea, Ashley Cole, mwenye umri wa miaka 43, ananyatiwa na timu mbalimbali zinazoshiriki Ligi ya Championship. ***(Mirror)***

### CHELSEA KUSAJILI MABEKI

KLABU ya Chelsea inatarajia kusajili mshambuliaji na mabeki wawili msimu huu wa joto huku wakurugenzi wa michezo wa klabu hiyo, Paul Winstanley na Laurence Stewart, wakiwa katika mpango ya kukabidhiwa tena majukumu yao ya uhamisho. ***(Telegraph)***

### THURAM ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL imepewa nafasi ya kumsajili kiungo wa kati wa Nice na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Khephren Thuram, mwenye umri wa miaka 23 kwa pauni milioni 13 msimu huu. ***(Mirror)***

### SLOT KUMBEBA HULSHOFF

KOCHA wa Feyenoord, Arne Slot, anapanga kumfanya msaidizi wake, Sipke Hulshoff, kuwa sehemu ya benchi la ufundi katika kikosi cha Liverpool baada ya kukubali mikoba ya Jurgen Klopp. ***(ESPN)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KANTE AJUMUISHWA KIKOSI CHA UFARANSA

●●●Nyota huyo alikuwa nje ya timu hiyo tangu mwaka 2022...

**PARIS, Ufaransa**

KOCHA wa Ufaransa, Didier Deschamps, amemjumuisha kiungo wa kati, N'Golo Kanté, katika orodha yake ya awali ya wachezaji kwa ajili ya michuano ya Euro 2024 na amemwita kwa mara ya kwanza mshambuliaji wa Paris Saint-Germain, Bradley Barcola.

Kurejea kwa Kanté hakukutarajiwa kufuatia mchezaji huyo wa zamani wa Chelsea kwenda katika Ligi ya Saudia msimu uliopita baada ya kusumbuliwa na majeraha. Mshindi huyo wa Kombe la Dunia 2018 hajaichezea Ufaransa tangu Juni 2022.

Deschamps alisema Kanté amerudisha kiwango chake katika klabu ya Al-Ittihad.

„Amekuwa na msimu mzima, ingawa si katika Ligi ya Ulaya, anacheza nchini Saudi Arabia, ambako amerejesha utimamu wake wa mwili," alisema Deschamps alipokuwa akitangaza kikosi chake katika Kituo cha televisheni cha Ufaransa TF1.

„Na nadhani kwa uzoefu wake na historia yake, nina imani timu yetu itakuwa na nguvu zaidi naye."

Uwepo wa Barcola kikosini ulitarajiwa na wengi kufuatia msimu wake bora akiwa na PSG.

Baada ya kujiunga akitokea Lyon, winga huyo mwenye umri wa miaka 21, mwenye kasi nzuri na ujuzi wa kuchezea chenga ametulia haraka katika klabu hiyo yenye nyota wengi. Alicheza mechi kubwa na ndiyo sababu kuu ya PSG kufanikiwa kuwapita Barcelona katika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa.

Beki wa kushoto wa Real Madrid, Ferland Mendy, ambaye hajaichezea Ufaransa tangu Septemba 2022, pia amerejea.

Beki wa PSG, Lucas Hernández, ambaye hivi majuzi alifanyiwa upasuaji baada ya kupasuka goti la kushoto ameachwa.

Deschamps bado anaweza kurekebisha kikosi chake kabla ya tarehe ya mwisho ya Juni 7, mwaka huu.

Michuano hiyo itafanyika kuanzia Juni 14, mwaka huu nchini Ujerumani.

Ufaransa bingwa mara mbili ipo Kundi D pamoja na Austria, Uholanzi na Poland.

Kikosi Kamili:

Makipa: Alphonse Areola (West Ham), Mike Maignan (AC Milan), Brice Samba (Lens)

Mabeki: Jonathan Clauss (Marseille), Theo Hernández (AC Milan), Ibrahima Konaté (Liverpool), Jules Koundé (Barcelona), Ferland Mendy (Real Madrid), Benjamin Pavard (Inter Milan), William Saliba (Arsenal), Dayot Upamecano ( Bayern Munich).

Viungo: Eduardo Camavinga (Real Madrid), Youssouf Fofana (Monaco), Antoine Griezmann (Atlético Madrid), N'Golo Kanté (Al-Ittihad), Adrien Rabiot (Juventus Turin), Aurélien Tchouaméni (Real Madrid), Warren Zaïre-Emery (PSG).

Washambuliaji: Bradley Barcola (PSG), Kingsley Coman (Bayern Munich), Ousmane Dembélé (PSG), Olivier Giroud (AC Milan), Randal Kolo Muani (PSG), Kylian Mbappé (PSG), Marcus Thuram (Inter Milan).

HABARI MICHEZO

# Ederson kuikosa fainali FA

**MANCHESTER, England**

EDERSON atakosa mechi ya mwisho ya Manchester City ya Ligi Kuu England pamoja na fainali ya Kombe la FA kutokana na kuvunjika mzunguko wa jicho la kulia.

Taarifa ya Manchester City ilisema, Ederson alifanyiwa vipimo baada ya kupata jeraha wakati alipogongana na Cristian Romero katika ushindi wa 2-0 dhidi ya Tottenham Hotspur Jumanne.


Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil alicheza kwa muda mfupi lakini hatimaye akaondolewa, na badala yake, Stefan Ortega, akaokoa hatari kutoka kwa Dejan Kulusevski na Son Heung-Min.

"Jeraha hilo litamzuia Ederson kucheza sehemu nyingine katika michezo iliyosalia ya msimu wa 2023-24," taarifa ya City ilisema.

City itacheza na West Ham nyumbani kesho na wanahitaji ushindi ili kujihakikishia taji la nne mfululizo la Ligi Kuu.

Baada ya mechi hiyo, kikosi hicho cha Pep Guardiola kitacheza na Manchester United katika mchezo wa fainali ya Kombe la FA utakaofanyika Mei 25, mwaka huu.

Ederson alichaguliwa wiki iliyopita katika kikosi cha Brazil kwa ajili ya Copa América nchini Marekani itakayoanza Juni na kumalizika Julai.




# RONALDO AONGOZA ORODHA WANAOLIPWA FEDHA NYINGI

**NEW YORK, Marekani**

CRISTIANO Ronaldo ameongoza orodha ya Jarida la Forbes ya wanamichezo wanaolipwa fedha nyingi zaidi duniani kwa mara ya nne katika maisha yake ya soka, huku Jon Rahm mcheza gofu akipanda hadi nafasi ya pili.

Ronaldo pia aliongoza orodha hiyo mwaka jana baada ya kuhamia klabu ya soka ya Saudi Arabia ya Al Nassr.

Jarida la biashara la Forbes la Marekani limesema, mshambuliaji huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 39 amepata kiasi cha Dola za Marekani milioni 260 kutoka Dola Marekabi milioni 136 katika kipindi cha miezi 12 iliyopita.

Mpinzani mkubwa wa Ronaldo, Lionel Messi, ameshuka hadi nafasi ya tatu katika orodha hiyo akiwa ameingiza Dola milioni 135.

Mchezaji gofu wa Hispania Rahm amepanda hadi nafasi pili akipata baada ya kuvuna Dola milioni 218.

Mcheza gofu huyo ni mmoja wa wanamichezo 22 walio na umri wa chini ya miaka 30 kwenye orodha hiyo.

Wanamichezo waliodumu katika hiyo orodha kama vile Serena Williams, Roger Federer na Tom Brady tayari wamestaafu, wakati Ronaldo, LeBron James, Tiger Woods na wengine watatu wenye umri wa miaka 39 au zaidi, pia nao wakitarajiwa kuchukua hatua hiyo hivi karibuni.

Wanasoka Neymar na Karim Benzema pia wameingia katika 10 bora baada ya kuhamia katika Saudia.

Giannis Antetokounmpo (katika nafasi ya tano) anaungana na nyota wenzake wa mpira wa kikapu, LeBron James (wa nne) na Stephen Curry (wa tisa) kwenye orodha hiyo, huku Lamar Jackson anayecheza mpira wa magongo wa Marekani akiwa katika nafasi ya 10.

Kwa mujibu wa Forbes, wanamichezo 10 wanaolipwa zaidi duniani kwa pamoja walipata jumla ya Dola Bilioni 1.38 kabla ya ushuru na ada za mawakala katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, ambayo ni jumla ya juu zaidi kuwahi kutokea.

Katika nafasi ya 14, Canelo Alvarez bondia ambaye alikulia katika maisha ya umaskini wa mashambani na alianza kupigana akilipwa dola 40, anakadiriwa na Jarida la Forbes kuna na thamani ya angalau dola milioni 275 milioni.

Katika nafasi ya 16 ni bondia wa uzito wa juu duniani Anthony Joshua kutoka Uingereza anayedaiwa kuwa na thamani ya dola milioni 83.

Mshambuliaji wa Manchester City, Erling Halaand ambaye ameorodheshwa katika nafasi ya 27 ana thamani ya dola milioni 61.

Mchezaji soka kutoka Afrika anayelipwa fedha nyingi zaidi ni Mohammed Salah kutoka Misri mwenye thamani ya dola milioni 53. Salah anashikilia nafasi ya 38.

Nyuma yake ni Sadio Mane mshambuliaji wa Senegal mwenye thamani ya dola milioni 52 katika nafasi ya 40.

Ifuatayo ni orodha ya wachezaji 10 wanaolipwa fedha nyingi zaidi duniani;




# Ujerumani yatema wakongwe Euro 2024

**BERLIN, Ujerumani**

WENYEJI wa Euro 2024, Ujerumani wametaja kikosi cha kwanza kwa ajili ya michuano hiyo, huku wakongwe Mats Hummels na Leon Goretzka wakiachwa.

Kocha wa Ujerumani, Julian Nagelsmann, amewaita magolikipa wanne katika kikosi hicho, huku Alexander Nübel wa VfB Stuttgart akiungana na Manuel Neuer, Oliver Baumann na Marc-André ter Stegen.

"Unapokuwa na muundo huu, ambao bado unakua lakini dhaifu baada ya maonyesho yetu Machi, unaleta vipengele vipya ili kusababisha muundo huo na itabidi uanze kutoka mwanzo," alisema Nagelsmann.

Mabingwa mara tatu wa Ulaya, Ujerumani ambao hawajashinda taji lolote kubwa tangu Kombe la Dunia 2014, walishinda dhidi ya Ufaransa na Uholanzi katika mechi za kirafiki mfululizo Machi, matokeo yao bora kwa muda mrefu.

Nagelsmann alisema kuwa na makipa wanne ni muhimu wakati wa mashindano.

"Tumeteua makipa wanne na tutakwenda na wanne katika michuano hiyo. Nübel amestahili kuteuliwa," aliongeza Nagelsmann.

"Kwa nini walinda mlango wanne? Unaweza kuwa na makipa katika mazoezi pia na Manuel Neuer sio lazima afanye hivyo kila wakati.

"Hiyo inamaanisha wachezaji 22 wa ndani. Ninaweza kuishi na hilo vizuri sana. Bado tunaweza kufanya mazoezi yanayofaa na angalau wachezaji 20 wa ndani ikiwa wengine watakosekana."

Katika wakongwe Thomas Müller, Toni Kroos na Neuer, kuna mabingwa watatu wa dunia wa 2014 katika kikosi cha wachezaji 27 ambao lazima wapunguzwe hadi 26 kabla ya michuano hiyo.

Aleksandar Pavlovic mwenye umri wa miaka 20, ambaye alikosa mechi za kirafiki za Machi kutokana na jeraha bado anasubiri mechi yake ya kwanza, na alikuwa na kiwango bora zaidi kwa Bayern Munich.

Robert Andrich, Florian Wirtz na Jonathan Tah ni wachezaji wa Bayer Leverkusen katika kikosi ambao wamesaidia mabingwa hao wa Bundesliga.

Ujerumani itaanza kampeni ya Kundi A katika mechi ya ufunguzi wa michuano hiyo dhidi ya Scotland Juni 14.

Pia itacheza na Hungary na Uswiswi katika kundi hilo.

HABARI MICHEZO

# AZIZ KI HATARI KWA FRI-KIKI, KYOMBO MAGOLI YA VICHWA

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara,Yanga, Stephane Aziz Ki, anayeongoza kwa kufunga mabao, ameweka rekodi nyingine ya kuwa kinara wa kupachika mabao kwa mipira ya adhabu ,fri-kiki', mpaka sasa.

Kwa mujibu wa takwimu ziliyotolewa na Bodi ya Ligi jana, pamoja na za dawati letu la michezo, Aziz Ki, mwenye mabao 15 katika Ligi Kuu, akiwa sambamba na Feisal Salum, amepachika mabao tatu kwa njia ya faulo, na kuwa mchezaji aliyefunga mabao mengi ya aina hiyo kwenye Ligi Kuu, wakati zimebakia raundi tatu tu kumalika.

Raia huyo wa Burkina Faso ambaye pia ni mmoja wa wanaoongoza kwa kutoa pasi za mwisho za mabao, akifanya hivyo mara nane, pamoja na Kipre Junior na Fei Toto, wote wa Azam, amekuwa na rekodi nyingi nzuri msimu huu, ikiwamo kuongoza kwa kupachika mabao akiwa nje ya boksi, ambapo amefanya hivyo mara tano.

Wakati Aziz Ki, akiwa na mabao matatu ya faulo, nyuma yake yupo Edwin Balua wa Simba ambaye ana mabao mawili ya ,fri-kiki', moja akilifunga akiwa na timu yake ya zamani Prisons, akifunga timu yake ya sasa, na moja akiwa kwenye klabu yake mpya akifunga dhidi ya Namungo. Mwingine mwenye mabao mawili, ni raia wa Togo, anayewindwa kwa sasa na Simba, Marouf Tchakei wa Ihefu.

Wachezaji waliofunga bao moja la faulo ni, Cheikh Sidibe wa Azam FC, Gadiel Michael wa Singida Fountain Gate, Valentino Mashaka wa Gaita Gold, Ibrahim Ajibu wa Coastal Union, Clatous Chama wa Simba, Martin Kigi na Najimu Magulu wote wa JKT Tanzania, Jeremiah Juma wa Prisons, Dissan Galiwango na David Luhende, wote wa Kagera Sugar, na Omari Kindamba wa Mashujaa FC.

Takwimu zinaonyesha straika wa Singida Fountain Gate, Habib Kyombo, anaongoza kwa kupachika mabao ya vichwa mpaka sasa, akiwa ameshatumbukiza magoli

manne.

Mchezaji huyo anafuatiwa na wachezaji waliopachika mabao matatu ya kujitwisha, ambao ni Sadio Kanoute wa Simba, Waziri Junior (KMC), Paul Buswita (Namungo), Elvis Rupia wa Ihefu FC, na Semfuko Charles wa Coastal Union.




Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia (katikati), Makamu wa Rais wa shirikisho hilo, Athumani Nyamlani (kulia) na Katibu Mkuu wao, Wilfred Kidao wakiwa katika Mkutano Mkuu wa FIFA unaofanyika Bangkok, Thailand. **PICHA: MTANDAO**

# Mashindano Akili Bandia yanukia

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

KILELE cha Mashindano ya Ubunifu wa Akili Bandia Afrika yamepangwa kufanyika kuanzia Oktoba 13 hadi 17, mwaka huu jijini, Dar es Salaam.

Mashindano hayo yatashirikisha vijana wabunifu ambao watatengeneza maroboti yatakayotumika kufanya kazi mbalimbali.

Akizungumza jijini jana, Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia, Mohamed Abdullah, alisema lengo la mashindano hayo ni kutaka vijana kwenda na teknolojia za kisasa lakini pia kuhimiza matumizi ya TEHAMA.

Abdullah alisema vijana wote wenye nia nzuri ya kushiriki katika mashindano hayo wanatakiwa kufanya hivyo ili kujiongezea ujuzi katika masuala ya teknolojia mpya ambayo inahimizwa matumizi ya TEHAMA.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha vijana wanabadilika katika matumizi ya TEHAMA na kuongeza hawataki kuona vijana wanabaki nyuma.

Aliongeza siku hiyo kutakiwa na roboti za aina mbalimbali zitakazoonyeshwa kwa watu watakaoshiriki katika mashindano hayo huku Dola za Marekani 100,000 zimetolewa kwa ajili ya washindi.

## Yanga, Azam FC hesabu FA Cup

INATOKA UK. 24

(Simba), Kelvin Sabato (Namungo), George Chande (TMA Stars), Francis Joseph (Mwajuni FC), George Komba (Rhino Rangers), Shaaban Seif (Mbuni FC) na Wagana Paskas wa Biashara United ya Mara.

Simba ambao ilibeba Ngao ya Jamii na ubingwa wa mashindano ya Kombe la Muungano iliondolewa katika michuano hiyo ya Mashujaa FC ya Kigoma.

## Simba yagomea dau la Chama

INATOKA UK. 24

ka na ofa yao watahakikisha wanambakiza na asiyeridhika watampa baraka zote aende atakapopata kile anachokihitaji.

Pia niseme tuko katika vita vya kusaka nafasi ya pili lakini hii haitatufanya tusianze kuangalia mahitaji yetu kwa wachezaji wapya ambao tutawasajili, fedha ipo tunaenda sokoni kuangalia mahitaji yetu kwa kufuata mapendekezo ya benchi la ufundi ili kuimarisha timu yetu kuelekea msimu mpya," alisema Ahmed.

Bao la dakika ya saba la Muivory Coast, Freddy Michael, jana liliifanya Simba kufufua matumaini yake ya kucheza michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao, ikitoka na ushindi wa goli 1-0 dhidi ya Dodoma Jiji, mchezo ukipigwa Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Ushindi huo umewafanya Wekundu wa Msimbazi, kufikisha pointi 60 sawa na Azam FC, zote zikicheza mechi 27, lakini bado inaendelea kusota katika nafasi ya tatu ya msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, kutokana na kuwa na uwiano mdogo wa mabao ya kufunga na kufungwa.

Bao hilo pia, linamfanya straika huyo aliyesajiliwa kipindi cha uhamisho wa dirisha dogo la mwezi Januari, kufikisha mabao sita katika orodha ya wafungaji wa mabao msimu huu.

Freddy alifunga bao hilo kwa shuti la mguu wa kulia, baada ya pasi nzuri mpenyezo kutoka kwa Edwin Balua.

Awali beki wa Dodoma Jiji, Joram Mgeveke aliuokoa mpira kwa kichwa ambao ulimkuta Fabrice Ngoma, katikati ya uwanja, akapiga pasi ndefu kwa Balua, ambaye aliipeleka upande wa kulia alikokuwa mfungaji, aliyeachia shuti kali akiwa karibu na lango, lililomshinda kipa Aron Kalambo na kujaa wavuni.

Katika mechi ya jana, Simba iliuanza mchezo kwa kasi na kufika langoni mwa Dodoma Jiji, lakini mashambulizi yao yalikuwa mepesi, kabla kibao hakijageuka dakika ya pili ya mchezo.

Shambulio la kwanza la Dodoma Jiji lilikuwa kali na nusura lizae bao kama si uhodari wa kipa Hussein Abel, aliyeruka juu ya kuupangua mpira wa krosi ya Emmanuel Martin ambayo ilionekana kutaka kuingia moja kwa moja wavuni.

Kama vile haitoshi, dakika moja baadaye, Abel, aliyekuwa kwenye kiwango cha juu jana, ikiwa ni mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu msimu huu na kutoka na ,clean sheets', alilazimika kujitosa kwenye miguu ya Paul Peter kuudaka mpira ambao mchezaji huyo alikuwa anajiandaa kuupiga, wakibaki wao wawili tu.

# Michezo

Jumamosi Mei 18, 2024

Nipashe


## Ederson kuikosa fainali FA

UKURASA 22





Mshambuliaji wa Simba, Freddy Michael (jezi nyekundu), akipambana kuwania mpira dhidi ya wachezaji wa Dodoma Jiji katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri jana. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YAGOMEA DAU LA CHAMA

## ●●●Yafunguka iko tayari kuachana naye,yaikamata Azam FC....

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI Simba wakiendelea kuwapa mikataba mipya baadhi ya wachezaji wake, kiungo mshambuliaji wa timu hiyo Mzambia, Clatous Chama, amesema anahitaji kulipwa Dola za Marekani 300,000 ( zaidi ya Sh. milioni 765), ili akubali kusaini mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia klabu hiyo.

Taarifa zilizopatikana jijini, Dar es Salaam kutoka kwa Wekundu wa Msimbazi, Chama ameweka wazi anahitaji kiasi hicho cha fedha ili aendelee kuvaa jezi za rangi nyekundu na nyeupe katika mashindano mbalimbali msimu ujao.

Chanzo hicho kilisema Mzambia huyo amewaeleza mabosi wa Simba uamuzi wake huo katika kikao walichokutana naye ambao walihitaji kumaliza mchakato wa kumwongezea mkataba nyota huyo.

Taarifa zaidi zilisema Simba imegoma kumpatia Chama dau hilo kwa sababu ya umri wake na ilimpatia ofa ambayo wanaweza kumpa kiungo huyo ambaye alirejea tena Msimbazi akitokea RS Berkane ya Morocco.

„Chama amesema anataka kulipwa Dola 300,000 ili aendelee kubakia Simba, lakini viongozi wamesema hawawezi kutoa kiasi hicho kwa mchezaji wa umri wake. Wamempa ofa yao na endapoataridhika atasaini mkataba mwingine wa miaka miwili,“ kilisema chanzo chetu.

Kiliongeza kuwa kama Chama ataendelea kushikilia uamuzi wa kulipwa dau hilo alilotamka, Simba itakuwa tayari kumwacha aende kujiunga na klabu nyingine.

“Wamempa ofa yao (bila kutaja kiasi), baada ya kugoma kumpa ofa aliyoileta rasmi mezani, unajua ni zaidi ya milioni 600, na wamemwambia kama ataendelea na msimamo huo, wamemwambia hawataweza kuendelea naye,” kiliongeza chanzo chetu.

Habari zaidi zinasema Simba imedhamiria kuboresha kikosi chake na hii ni kuhakikisha wanafikia malengo ya kufanya vizuri katika mashindano yote watakayoshiriki msimu ujao.

„Tutasajili kweli, usajili hautakuwa wa kitoto, kuna wachezaji ambao tayari mazungumzo yamekamilika na wengine wanaendelea nao, nyota hao baadhi watatoka klabu za hapa ndani na wachache ni wa kutoka nje ya Tanzania.

Kwa sasa mazungumzo yanayoendelea ni baina yao na uongozi wa Ihefu kwa ajili ya kupata huduma ya kiungo, Marouf Tchakie, ambapo wametakiwa kutoa Dola za Marekani 50,000,“ alisema mtoa habari wetu.

Taarifa ziliongeza pia kuna mazungumzo yanaendelea ya kumpeleka Luis Miquissone katika kikosi cha Ihefu.

Nipashe lilimtafuta Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema mchakato wa usajili wa wachezaji unaendelea kwa umakini na utulivu kwa sababu wanataka kurejesha furaha kwa wanachama na mashabiki wao.

Ahmed alisema pia bado wanaendelea kujipanga kuhakikisha wanamaliza msimu ujao katika nafasi ya pili ili kujihakikishia tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

„Kuna baadhi ya wachezaji tayari wameshaongezewa mikataba na wengine wapo katika mazungumzo, atakayeridhi-

INAENDELEA UK. 23

## Yanga, Azam FC hesabu FA Cup

**Na Somoe Ng'itu**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi na Yousuopha Dabo wa Azam FC, kila mmoja amesema kikosi chake kiko tayari kwa ajili ya mechi za hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA itakayochezwa leo na kesho.

Azam FC inatarajia kuivaa Coastal Union katika mechi ya nusu fainali ya kwanza itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza wakati mabingwa watetezi wa michuano hiyo, Yanga watawavaa Ihefu ndani ya dimba la Sheikh Amri Abeid, Arusha.

Gamondi aliliambia gazeti hili wataingia kwa tahadhari katika mchezo huo kwa sababu mara zote hukutana na ushindani wanacheza dhidi ya Ihefu.

Kocha huyo alisema hakuna mechi rahisi ya hatua ya robo fainali kwa sababu timu zote zilizosonga mbele ni nzuri na zina wachezaji wenye uzoefu.

„Itakuwa mechi yenye ushindani, tunahitaji kupambana ili kupata matokeo mazuri, wapinzani wetu wamekuwa na wakati mzuri zaidi kila tunapokutana, hatutawadharau,“ alisema Gamondi.

Naye Dabo alisema wachezaji wake wako tayari kwa ajili ya mechi hiyo na wataingia kuwavaa kwa umakini.

Kocha huyo alisema mechi za mtoano huwa ngumu kwa sababu timu moja inatakiwa kusonga mbele na nyingine kuendelea na mashindano husika.

„Tunatarajia mechi itakuwa na ushindani wakati wote, tumebaki timu nne, mbili zitaendelea na nyingine zitatoka, ni lazima uwe bora ili upate nafasi ya kusonga mbele, hatutarajii kukutana na mechi rahisi,“ Dabo alisema.

Wakati huo huo mshambuliaji wa Yanga, Clement Mzize na straika wa JKT Tanzania, Edward Songo, wanaongoza katika orodha ya kufunga mabao, kila mmoja amepachika wavuni magoli matano.

JKT Tanzania, imeshatolewa katika mashindano hayo na hiyo itamfanya Songo kutopata nafasi ya kuendelea kufunga.

Wachezaji wanaofuata ni Yohana Mkomola kutoka Tabora United ambaye amefunga mabao manne huku waliotikisa nyavu za wapinzani mara tatu kila mmoja ni pamoja na Joseph Guede wa Yanga, Sadio Kanoute

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >